## JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
## OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, 16 Barabara ya Samora Machel, S. L.P. 9080, 11101 Dar Es Salaam.
Simu: 255(022)2115157/8, Fax: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

# Muhtasari wa matokeo ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016

Taarifa kwa Vyombo vya Habari kuhusu Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2016

**Prof. Mussa Juma Assad**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

**13 Aprili, 2017**

## YALIYOMO


UWASILISHAJI WA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA......... 5

SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 BUNGENI ........................................... 5

1.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ........................................................ 7

1.1 HATI ZA UKAGUZI........................................................................ 7

1.2 HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA MIAKA ILIYOPITA........................................................................ 7

1.3 MAPUNGUFU YALIYOBAINIKA WAKATI WA UKAGUZI WA HESABU ZA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 ........................................................ 8

2.0 USIMAMIZI WA MAPATO YATOKANAYO NA KODI ................................... 8

2.1 MATUMIZI MABAYA YA MSAMAHA WA KODI SHILINGI BILIONI 3.46............. 9

2.2 TATHMINI YA UDHIBITI WA MISAMAHA YA MAFUTA YANAYOINGIZWA NCHINI KWA AJILI YA MATUMIZI YA MIGODI ........................................ 9

2.3 KODI YA THAMANI YA SHILINGI BILIONI 4.87 ISIYOTHIBITIKA KULIPWA ... 9

2.4 USAMBAZAJI WA MACHINE ZA EFD.................................................10

2.5 USIMAMIZI NA UFUATILIAJI USIORIDHISHA WA MADENI YA KODI NA TOZO TZS 613.6 BILIONI ........................................................................10

2.6 USIMAMIZI WA MAKUSANYO YASIYOTOKANA NA KODI ..........................11

2.7 UANDAAJI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI ...........................................12

2.8 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO KUGHARAMIA MATUMIZI ..........13

3.0 USIMAMIZI WA DENI LA TAIFA.......................................................13

3.1 HALI YA DENI LA TAIFA................................................................13

3.2 UCHELEWESHWAJI MICHANGO YA KISHERIA KWENYE MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII-SHILINGI BILIONI 284 ................................................15

4.0 USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU.....................................................15

4.1 MALIPO YA MISHAHARA YA SHILINGI BILIONI 7.3 NA MAKATO YA KISHERIA YA SHILINGI BILIONI 2.5 YALIFANYIKA KWA WATUMISHI WALIOACHA KAZI AU KUFARIKI......................................................................................16

4.2 KUSHINDWA KUJIRIDHISHA KUHUSU UREJESHWAJI WA MISHAHARA KATIKA AKAUNTI YA HAZINA SHILINGI BILIONI 4.33 ..................................16

4.3 MALIMBIKIZO YA MADAI YA WAFANYAKAZI KIASI CHA SHILINGI BILIONI 14.4 17

4.4 WAKUU WA VITENGO KUKAIMU NAFASI ZILIZO WAZI KWA KIPINDI CHA ZAIDI YA MIEZI SITA.......................................................................17

5.0 USIMAMIZI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA SERIKALI ...................................17

5.1 MATUMIZI YASIYOKUWA NA MANUFAA KWA SERIKALI SHILINGI BILIONI 2.02 17

5.2 KUKOSEKANA KWA NYARAKA ZINAZOTHIBITISHA MATUMIZI YA HAMISHO LA FEDHA LA SHILINGI BILIONI 6.57 ....... 18

5.3 MAPUNGUFU KATIKA NYARAKA ZA MALIPO YA SHILINGI BILIONI 22.7 ....... 18

6.0 USIMAMIZI WA MALI NA MADENI YA SERIKALI ....... 18

6.1 UWEPO WA MALI ZA KUDUMU ZILIZOTELEKEZWA ....... 18

6.2 DAWA ZILIZOKWISHA MUDA WA MATUMIZI AMBAZO HAZIJAHARIBIWA SHILINGI BILIONI 10.19 ....... 19

6.3 UKARABATI WA MAJENGO YA SERIKALI NA UENDELEZWAJI WA VIWANJA VYA SERIKALI KATIKA BALOZI ZA TANZANIA NJE YA NCHI ....... 19

6.4 MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAMILIKA YENYE THAMANI YA SHILINGI BILIONI 4.2 AMBAYO HAITUMIKI ....... 19

7.0 USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA ....... 20

8.0 UKAGUZI WA VYAMA VYA SIASA ....... 20

9.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA ....... 21

9.1 BENKI YA WANAWAKE TANZANIA. ....... 21

9.2 BENKI YA TWIGA ....... 21

9.3 SHIRIKA LA USAMBAZAJI WA UMEME TANZANIA (TANESCO) ....... 22

9.4 MIFUKO YA PENSHENI ....... 22

9.5 MAMLAKA YA BANDARI TANZANIA ....... 23

9.6 UKAGUZI WA SEKTA YA MADINI ....... 23

9.7 MAKAMPUNI YA MADINI KUTENGENEZA HASARA KWA MUDA MREFU ....... 24

9.8 KUENDELEA KUTOZA KODI KWA KIWANGO CHA CHINI IKILINGANISHWA NA VIWANGO VINAVYOTOZWA SASA ....... 25

9.9 UBIA KATI YA STAMICO NA TML ....... 25

9.10 TATHMINI YA UENDESHAJI MGODI WA STAMIGOLD - BIHARAMULO ....... 26

9.11 UKAGUZI WA MAFUTA NA GESI; ....... 26

10.0 MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU ....... 28

10.1 UKAGUZI MAALUMU WA MAMLAKA YA VITABULISHO VYA TAIFA ....... 28

10.2 UKAGUZI MAALUM WA FEDHA ZA GAVI ALLIANCE KWA AJILI YA CHANJO YA SURUA RUBELLA ....... 28

11.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA UFANISI ....... 30

11.1 HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI ....... 30

11.3 RIPOTI UKAGUZI WA UFANISI KATIKA UZALISHAJI WA WAHITIMU KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA ....... 33

11.4 RIPOTI YA UKAGUZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MSINGI ....... 35

**11.5 RIPOTI YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU UDHIBITI WA UENDELEZAJI WA MAENEO YA WAZI YAALIYOAINISHWA NCHINI ........................................................................36**

**11.6 UKAGUZI WA UFANISI KATIKA USIMAMIZI WA USALAMA DHIDI YA MOTO KATIKA MAJENGO YA UMMA ..........................................................................................................37**

**11.7 USIMAMIZI WA MIKATABA ILIYOINGIWA KATI YA SERIKALI NA HOSPITALI ZA BINAFSI NCHINI ..............................................................................................................................39**

**11.8 UKAGUZI WA UFANISI KATIKA USIMAMIZI WA SAMANI ZA BARABARANI .....41**

**11.9 USIMAMIZI WA UCHUKUAJI WA MAJI KUTOKA KATIKA VYANZO VYA MAJI ...42**

**11.10 USIMAMIZI WA KAGUZI ZA VYOMBO VYA MAJINI KWA AJILI YA KUPEWA VYETI VYA UBORA NA KUKIDHI VIWANGO VYA USALAMA WA USAFIRISHAJI ........45**

**UWASILISHAJI WA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 BUNGENI**

**Ndugu Wanahabari,**

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) inanielekeza niwasilishe kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kila taarifa nitakayoitoa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo (2) ya ibara hii. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe tarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakaachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo, tendo ambalo limefanyika leo tarehe 13/04/2017

Kufuatia wajibu huo wa Kikatiba, napenda kuwafahamisha kuwa ripoti zifuatazo za ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016 ziliwasilishwa kwa wakati kwa Mh. Rais na leo hii kuwasilisha Bungeni na Mawaziri husika: (i) Ripoti ya Serikali Kuu; (ii) Ripoti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; (iii) Ripoti ya Mashirika ya Umma; (iv) Ripoti ya Miradi ya Maendeleo; (v) Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi; na (vi) Ripoti 9 zinazohusu sekta mbalimbali zilizofanyiwa Ukaguzi wa Ufanisi.

**Ndugu Wanahabari,**

Kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2016 nimefanya ukaguzi na kutoa ripoti kwa jumla ya Taasisi 543 ambazo ni; Taasisi za Serikali Kuu 222; Serikali za Mitaa 171; Mashirika ya Umma 150 kati ya 200. Katika Taasisi hizo pia, nimekagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kutoa ripoti 797. Kuhusu taarifa za ukaguzi wa ufanisi zilizotolewa zimegawajika katika maeneo yafuatayo;

| SNo. | RIPOTI |
|---|---|
| 1. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Uzalishaji wa Wahitimu katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.** (*Performance Audit Report on the Produced Graduates in Oil and Natural Gas Industry)* |
| 2. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Miundombinu ya Shule za Msingi Tanzania** (*Performance Audit Report on the Availability and Upkeeping of Primary Schools' Infrastructure in Tanzania)* |
| 3. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Udhibiti wa Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi Yaliyo Ainishwa Nchini Tanzania** (*Performance Audit Report on the Enforcement of Development Control for the Planned Public Open* |

| SNo. | RIPOTI |
|---|---|
| | *Spaces In Tanzania)* |
| 4. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Usalama Dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma** *(Performance Audit Report on the Enforcement of Fire Safety in Public Buildings)* |
| 5. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Samani za Barabarani** *(Performance Audit Report on the Management of Roads Furniture)* |
| 6. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Kaguzi za Vyombo vya Majini kwa ajili ya Kupewa Vyeti vya Ubora na Kukidhi Viwango vya Usalama wa Usafirishaji (*Performance Audit Report on the Management of Surveys and Inspections of Vessels in Maritime Transportation)*** |
| 7. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Uchukuaji wa Maji kutoka Vyanzo vya Maji.** *(Performance Audit Report on the Control of Water Abstraction from the Water Sources)* |
| 8. | **Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Mikataba Iliyoingiwa kati ya Serikali na Hospitali za Binafsi Nchini.** *(Performance Audit Report on the Management of Hospital Agreements Between the Government and Private Hospitals)* |
| 9. | **Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi katika Taarifa Tano za Ukaguzi wa Ufanisi zilizotolewa na kusomwa Bungeni kuanzia mwaka 2012 hadi 2013.** *(Follow-up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations for the Five Performance Audit Reports Issued and Tabled to Parliament between 2012 and 2013)* |

**Ndugu Wanahabari,**
Baada ya kukabidhi ripoti hizi, naomba kutumia fursa hii kuelezea kwa ufupi mambo muhimu yaliyomo katika ripoti zilizowasilishwa Bungeni leo kama ifuatavyo:

## 1.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU

### 1.1 Hati za Ukaguzi

**Ndugu Wanahabari,**
Katika ukaguzi wa Hesabu nilioufanya katika mwaka wa fedha 2015/2016 nimetoa jumla ya Hati 505, zinazohusu usahihi wa Hesabu zilizoandaliwa na mihimili mitatu ya dola ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Kati ya hizo, Hati zinazoridhisha ni 436 (86.34%); Hati zenye shaka ni 60 (11.88%); Hati zisizoridhisha ni nne (0.79%); na Hati Mbaya ni tano (0.99%).

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi wa Hesabu kwa mwaka 2015/2016**

| Aina ya Ripoti | Jumla ya Hati | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha | Hati mbaya |
|---|---|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Serikali za Mitaa | 171 | 138 | 32 | 1 | 0 |
| Mashirika ya Umma | 112 | 108 | 4 | 0 | 0 |
| Serikali Kuu | 222 | 190 | 24 | 3 | 5 |
| ***Jumla*** | ***505*** | ***436*** | ***60*** | ***4*** | ***5*** |
| ***Asilimia*** | **100%** | **86.34%** | **11.88%** | **0.79%** | **0.99%** |

Aidha, katika ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 nimetoa hati za ukaguzi 797; ambapo Hati zinazoridhisha ni 725 (91%); Hati zenye shaka ni 71 (8.9%) na Hati mbaya ni moja (0.1%).

### 1.2 Hali ya utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita

**Ndugu Wanahabari,**
Katika ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa miaka iliyopita, nilitoa mapendekezo mbalimbali yanayolenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo hayo hairidhishi, kwani kati ya mapendekezo 234 yaliyotolewa, ni mapendekezo 32 (14%) yametekelezwa kikamilifu. Mchanganuo wa utekelezaji umeainishwa katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa miaka iliyopita**

| Aina ya Ripoti | Idadi ya Mapendekezo | Utekelezaji umekamilika | Utekelezaji unaendelea | Utekelezaji haujaanza |
|---|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Serikali za Mitaa | 79 | 03 | 35 | 41 |
| Mashirika ya Umma | 53 | 0 | 14 | 39 |
| Serikali Kuu | 102 | 29 | 53 | 20 |
| **Jumla** | **234** | **32** | **102** | **100** |
| ***Asilimia*** | **100%** | **14%** | **44%** | **42%** |

Utekelezaji wa mapendekezo ulikuwa ni mbaya zaidi kwa upande wa Serikali za Mitaa, kwani tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za miaka miwili ya fedha iliyopita (2012/13 na 2013/14) inaonesha kuwa kati ya mapendekezo 41 yaliyotolewa, mapendekezo 16 (39%) utekelezaji wake unaendelea na mapendekezo 25 (61%) utekelezaji wake haujaanza kabisa.

***Jitihada za Serikali zinahitajika katika kuhakikisha kuwa mapendekezo yanayotolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanatekelezwa kikamilifu ili kuleta tija katika usimamizi wa rasilimali za umma.***

## 1.3 Mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa Hesabu za mwaka wa Fedha 2015/2016

**Ndugu Wanahabari,**
Ukaguzi wa Hesabu kwa mwaka 2015/16, umebaini mambo kadhaa yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kuleta ufanisi na uwajibikaji katika kusimamia matumizi ya rasilimali za umma na ukusanyaji wa mapato kama ilivyoanishwa hapa chini:

## 2.0 USIMAMIZI WA MAPATO YATOKANAYO NA KODI

**Ndugu Wanahabari,**
Kwa mwaka ulioshia tarehe 30 Juni, 2016, makusanyo ya mapato yatokanayo na kodi yalipita malengo yaliyowekwa kwa asilimia 1, kutoka makisio ya shilingi bilioni 12,362.96 hadi kufikia makusanyo ya shilingi bilioni 12,509. Makusanyo hayo yanajumuisha misamaha ya kodi iliyotolewa kwa watumishi wa Umma kupitia manunuzi mbalimbali ya shilingi bilioni 25.69.

Pia Katika ukaguzi wangu wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, nimebaini mapungufu kadhaa yanayohitaji hatua madhubuti za Serikali ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi kama ifuatavyo:

### 2.1 Matumizi mabaya ya msamaha wa kodi Shilingi bilioni 3.46

Kupitia Taarifa ya Uchunguzi ya Tarehe 31 Mei, 2016 nilibaini matumizi mabaya ya msamaha wa kodi wa kiasi cha shilingi bilioni 3.46, ambao ulitolewa kwa walengwa wawili walioagiza jumla ya magari 238. Hata hivyo magari hayo yalisajiliwa kwa majina ya watu tofauti na wale waliopewa msamaha huo. Walengwa wote waliopewa misamaha hiyo walikana kuhusika na magari hayo, hali inayoonyesha kuwa bado kuna uhitaji wa kuboresha udhibiti na ufuatiliaji wa masuala ya misamaha ya kodi.

### 2.2 Tathmini ya udhibiti wa misamaha ya mafuta yanayoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya migodi

Katika ukaguzi huu nimebaini lita za mafuta 4,248,802 yaliyosafirishwa kutoka Dar es Salaam kati ya mwezi Oktoba 2014 na Disemba 2015 kwa ajili ya matumizi katika migodi ya Buzwagi, Bulyankulu na Geita. Hata hivyo, nyaraka za uthibitisho wa mafuta hayo kufika katika vituo husika hazikutolewa hali inayoashiria kuwa mafuta hayo yaliyosamehewa kodi yalitumika tofauti na yalivyokusudiwa.

Pia nibaini lita 20,791,072 za mafuta yenye msamaha wa kodi wa Shilingi bilioni 10.17 kwa ajili ya Mgodi wa Buzwagi kwa kipindi cha miezi 18 (kutoka Julai 2014 hadi Disemba 2015) yalisafirishwa kwenda kwa Kampuni ya M/S Aggreko mkandarasi msaidizi (sub-contractor) ambaye hakuwa mhusika katika msamaha huo.

***Naishauri Serikali (TRA) (a) kufanya uchunguzi wa mafuta yote ambayo hayana ushahidi kama yamesafirishwa katika vituo vya uchimbaji madini na kukusanya kodi inayodaiwa kiasi cha Shilingi bilioni 1.599; (b) kuhakikisha kodi ya Shilingi bilioni 10.17 katika mafuta yote yaliyosamehewa kodi na kupelekwa kwa wakandarasi wasiohusika na msamaha huo kama M/S Aggreko inakusanywa; na (c) kuhakikisha usimamizi unaimarishwa juu ya matumizi ya misamaha inayotolewa kwa mujibu wa sheria ili kuepusha hasara kwa Serikali kutokana na matumizi mabaya ya misamaha ya kodi hizo.***

### 2.3 Kodi ya thamani ya Shilingi bilioni 4.87 isiyothibitika kulipwa

Ukaguzi ulibaini kiasi cha lita 3,874,263 chenye kodi ya shilingi bilioni 2.45 kilichoingizwa nchini pasipo ushahidi wa taarifa za malipo ya kodi husika. Katika nyakati tofauti, sikupatiwa nyaraka za ukusanyaji wa kodi kiasi cha Shilingi bilioni 2.42 kutoka kwenye lita 3,234,420 za mafuta yaliyoingizwa

nchini na kampuni 24 za mafuta na kuchukuliwa na wamiliki kati ya tarehe 1 Januari hadi tarehe 30 Juni, 2016. Hii inaonesha mapungufu katika ukusanyaji wa kodi zitokanazo na uingizwaji wa mafuta.

***Nashauri Serikali ifanye uchunguzi ili kubaini usahihi wa matumizi ya mafuta hayo na pale itakapobainika hayakutumika ipasavyo, kodi husika zitozwe pamoja na riba. Pia, Serikali iboreshe mifumo ya kusimamia uagizaji wa mafuta ili kuzuia matatizo haya kujitokeza katika siku zijazo.***

### 2.4 Usambazaji wa Machine za EFD

Ukaguzi wangu ulibaini upungufu wa mashine za EFD kwa asilimia 84 ukilinganisha na mahitaji ya mashine hizo. Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2015 hadi Novemba, 2016 walipa kodi 8,165 kati ya 9,743 waliosajiliwa kulipa VAT hawakuwa na mashine za EFD.

***Nashauri Serikali iendelee kuhimiza matumizi ya mashine za EFD hasa kwa kuhakikisha wahusika wanachukua na kutumia mashine hizo kama kifungu cha 36 cha sheria ya usimamizi wa kodi ya mwaka 2015 na kanuni za EFD zinavyotaka.***

### 2.5 Usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa Madeni ya Kodi na Tozo TZS 613.6 Bilioni

Nimepitia orodha ya madeni ya Idara ya Uchunguzi, Idara ya Kodi za Ndani na Walipa Kodi Wakubwa pamoja na vielelezo vingine na kugundua jumla ya kodi kiasi cha shilingi bilioni 588.83 [Tax Investigation-TZS. 92.03 Bilioni; DRD-TZS 425.83 Bilioni na LTD –TZS 70.97 Bilioni] kilikuwa hakijakusanywa na Mamlaka kutoka kwa walipakodi mbalimbali. Hii inaonyesha udhaifu katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa madeni ya kodi na tozo.

Nilipitia pia sampuli ya majalada ya walipa kodi na kubaini kodi iliyokadiriwa na kukusanya na Mamlaka ya Mapato ilikuwa pungufu kwa jumla ya shilingi bilioni 9.45. Hii inaashiria kwamba Mamlaka haikufanya uchambuzi na upitiaji wa taarifa za mapato ya walipa kodi na vielelezo vyake (Tax Assessments and Reviews of Taxpayers' Income Tax and VAT Returns) ipasavyo. Hivyo, kutoa mwanya kwa wakadiliaji kufanya tathmini ndogo kwa walipa kodi na kuikosesha Serikali mapato.

Aidha, ukaguzi wa ukusanyaji wa kodi ya forodha umebaini Mamlaka haikukusanya (a) tozo za Maendeleo ya Reli ya jumla ya shilingi bilioni 9.27; (b) kodi ya bidhaa na mafuta na riba ya ucheleweshaji malipo ya shilingi bilioni 3.311; (c) ushuru wa forodha kiasi cha shilingi bilioni 9.319 kutokana na bidhaa 9,942,810 ambazo hazikuwepo kwenye maghala ya forodha; na (d)

kutokusanywa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye maziwa yaliyosindikwa shilingi bilioni 2.96 ambayo yaliingizwa nchini.

Hivyo jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 613.6 hakikusanywa na Mamlaka ingawa tathmini ya kodi ilifanyika kwa hoja zote nilizoeleza hapo juu.

***Ninaishauri Serikali kuimarisha mifumo yake na kuchukua hatua stahiki katika ukusanyaji wa kodi zilizokadiriwa hususani kwa wadaiwa sugu ikiwemo kutoza faini na kuweka riba katika ucheleweshaji wa malipo.***

## 2.6 USIMAMIZI WA MAKUSANYO YASIYOTOKANA NA KODI

**Ndugu Wanahabari,**

Mapato yasiyotokana na kodi yaliyokusanywa kutoka vyanzo vingine vya mapato kwa Serikali Kuu yalikuwa shilingi bilioni 1,613.99 sawa na asilimia 98.74, ikilinganishwa na makisio ya shilingi bilioni 1,634.56 hivyo kuwa na makusanyo pungufu ya shilingi bilioni 20.57 sawa na asilimia 1.3 ya makisio.

Kwa upande wa Serikali za Mitaa, jumla ya Shilingi bilioni 482.90 zilikusanywa kiasi hiki ni sawa na asilimia 90 ya makisio ya shilingi bilioni 536.20, hivyo kutofikiwa lengo la kukusanya shilingi bilioni 53.30 kwa asilimia 10.

Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo kuhusiana na mapato yasiyotokana na kodi kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa:

### 2.6.1 Makusanyo ya mapato yasiyowasilishwa na wakala wa Mapato kiasi cha shilingi bilioni 6

Ukaguzi umebaini kuwa mapato ya shilingi bilioni 6 hayakuwasilishwa na mawakala walioteuliwa kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri 80. Kwa upande mwingine, hapakuwa na dhamana iliyowekwa na mawakala hao endapo wangeshindwa kuwasilisha makusanyo hayo kwa mujibu wa mikataba waliyoingia na Halmashauri.

***Serikali inashauriwa hatua madhubuti kuhakikisha kwamba fedha zilizokusanywa na mawakala zinawasilishwa. Kwa mujibu wa mikataba iliyoingiwa baina yao na Mamlaka za Serikali za Mitaa Husika.***

### 2.6.2 Makusanyo ya mapato kutowasilishwa benki kiasi cha shilingi milioni 761.7

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri 33 hazikuwasilisha mapato yaliyokusanywa ya jumla ya shilingi milioni 761.7 kwenye akaunti za benki za Halmashauri husika; hii ikiwa ni kinyume na Agizo la 50 (5) la Mwongozo wa Fedha wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2009. Kutowasilisha makusanyo hayo kunaweza kupelekea matumizi ya makusanyo hayo kinyume na ilivyokusudiwa.

***Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zihimizwe kuzingatia Agizo la 50 (5) la Muongozo wa Fedha wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 ili kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato ya ndani.***

## 2.7 UANDAAJI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI

**Ndugu Wanahabari,**

Katika mwaka wa Fedha 2015/16 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 22,495.5 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 2,642.20 sawa na asilimia 13.13 ikilinganishwa na makisio ya shilingi bilioni 19,853.30 yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2014/15.

Mapato halisi yaliyokusanywa kutoka katika vyanzo vilivyoainishwa yalifikia shilingi bilioni 21,108.86 (sawa na asilimia 93.84 ya makadirio ya shilingi bilioni 22,495.5) ikionesha kushindwa kufikia lengo kwa jumla ya shilingi bilioni 1,386.64 (sawa na asilimia 6.16 ya makisio).

Kati ya shilingi bilioni 21,108.86 zilizokusanywa, shilingi bilioni 20,020.75 zilizotolewa kwa ajili ya Mishahara ya watumishi, matumizi mengineyo, matumizi ya shughuli za Maendeleo na matumizi ya Mfuko Mkuu. Matumizi ya kawaida na uendeshaji wa shughuli za Serikali yalifikia jumla ya shilingi bilioni 15,970.12 sawa na asilimia 79.77 wakati fedha za maendeleo zilifikia kiasi cha shilingi bilioni 4,050.83 sawa na asilimia 20.23. Hali hii inaonyesha kwamba sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali yalipelekwa kwenye matumizi ya kawaida kuliko shughuli za maendeleo.

## 2.8 Uchambuzi wa makadirio ya mapato kugharamia matumizi

Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka huku kukiwa na ongezeko kidogo katika ukusanyaji maduhuli kuweza kugharamia bajeti. Kuendelea kutegemea mikopo ya ndani na Nje kugharimia bajeti inaleta changamoto kwani mikopo huwa na riba ambayo itaanza kudhoofisha uchumi wakati wa kulipa madeni.

Sehemu ya bajeti ambayo ilifadhiliwa na mapato ya ndani ya nchi kutokana na kodi na yasiyotokana na kodi yalikuwa kiasi cha shilingi bilioni 14,007.52 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 22,495.5 ikionesha kwamba bila kutumia mikopo ya ndani, na nje na misaada, Serikali ingeweza kugharamia asilimia 62.58 tu ya bajeti yake hasa ukizingatia misaada kutoka kwa wahisani imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka. Hivyo kwa maoni yangu, Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali umekuwa chini ya makisio kwa kiasi kikubwa kitu ambacho kinapoteza sifa ya kuifanya Bajeti kuwa chombo cha muongozo na udhibiti kwenye utendaji wa Serikali.

.

***Serikali inapaswa kuandaa bajeti yenye uhalisia kwa maana kwamba, mapato ya ndani yawe na uwezo wa kugharamia bajeti kwa sehemu kubwa na kupunguza utegemezi kwenye mikopo hasa deni.***

# 3.0 USIMAMIZI WA DENI LA TAIFA

**Ndugu Wanahabari,**

## 3.1 Hali ya Deni la Taifa

Deni la Taifa kufikia tarehe 30 Juni, 2016 lilikuwa shilingi bilioni 41,039.39 [30 Juni 2015: bilioni 33,539.59] likiwa na ongezeko la bilioni 7,499.80 sawa na asilimia 22 ikilinganishwa na deni la mwaka uliopita. Aidha, kiasi hiki cha deni kilichoripoitiwa tarehe 30 Juni hakijajumlisha Shs. Bilioni 3,217 (sawa na 8% ya deni lililoripotiwa) ambayo ni madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii (TZS. 2,991.4 Billion) na madeni ambayo hayajalipwa na yanadhana ya Serikali (Expired Guarantees: TZS 225.6 Billion).

Hii inaashilia kuwa kiasi cha Deni la Taifa lililoripotiwa tarehe 30 Juni 2016 ni kidogo kuliko hali halisi. Ukaguzi imebaini kuwa Serikali imeshindwa kulijumuisha deni la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutokana na ucheleweshaji wa kutoa hati fungani (Non cash bond) ambazo Serikali iliahidi kuzitoa. Hivyo kukosekana kwa “instrument” inayomuwezesha Mhasibu Mkuu wa Serikali kuliingiza deni hili kwenye vitabu.

Aidha, Ukaguzi umebaini kuwa Deni la Taifa linakuwa kwa haraka kwa Zaidi ya asilimia 20[1] kwa mwaka ambayo kwa kiasi kikubwa kinatokana na mikopo ya biashara. Hivyo kusababisha marejesho ya deni na riba (debt service) kuongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na gharama za mikopo na muda mfupi wa urejeshwaji wake. Kwa kuangalia gharama za kuhudumia Deni la Taifa na kulinganishwa na mapato ya ndani, gharama hizo ziko juu ya viwango vinavyohitajika. Angalia Jedwali hapa chini linaloonyesha viashiria mbalimbali ya deni la taifa.

**Jedwali Na. 3: Viashiria vya Deni kwa miaka ishirini ijayo**

| External Public debt | Threshold | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2025 | 2035 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PV of debt to GDP | 50 | 20.9 | 19.9 | 23.5 | 22.9 | 21 | 20.2 | 20.9 | 18.4 |
| PV of debt to Exports | 200 | 104.4 | 97.7 | 99.2 | 96.9 | 95.7 | 99.3 | 98 | 89.5 |
| PV of debt to Revenue | 300 | 157.2 | 145.3 | 141.8 | 133.7 | 122.8 | 119.3 | 116 | 102.3 |
| Debt service to exports | 25 | 8.7 | 7.8 | 7.9 | 8.6 | 9.3 | 6.9 | 3.3 | 3 |
| Debt service to revenue | 22 | 13 | 11.5 | 11.4 | 11.9 | 11.9 | 8.3 | 4 | 3.5 |
| **Total Public debt** | | | | | | | | | |
| PV of public debt to GDP | **74** | 36.8 | 34.2 | 41 | 40.9 | 38.8 | 37.6 | 39.3 | 37.6 |
| PV of public debt to revenue | | 277.4 | 249.9 | 247 | 238.9 | 227.2 | 222.2 | 219.5 | 209.4 |
| Debt service to revenue ratio | | 23 | 30.8 | 27.9 | 32.9 | 47.5 | 28.2 | 27.5 | 31.1 |

**Chanzo: Taarifa ya Uhimilivu wa Deni la Taifa, 2016**

Kwa maoni yangu, kama ukuwaji huu ukiendelea kwa kiasi cha hivi sasa bila udhibiti madhubuti utaathiri uwezo wa Serikali kwenye matumizi ya maendeleo na mengineyo kwa miaka ijayo hasa ukizingatia Zaidi ya asilimia 80 ya mapato yake utumika kulipia Mishahara na Deni la Taifa.

Aidha, ukaguzi umebaini mapungufu katika usimamizi wa Deni la Taifa hii ikiwa pamoja na Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya mwaka 1974 (R.E. 2004) kuwa imepitwa na wakati; Kukopa Kabla ya Mapitio na Idhini ya Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Madeni (NDMC); kukopa kutoka benki za biashara ilikuwa kinyume na mpango wa uuzaji wa hati fungani wa mwaka 2015/16 ambao ulitaka Serikali kukopa ndani kwa kutoa hati fungani; na Muundo na Usimamizi wa Deni la Taifa nchini Tanzania umepitwa na wakati.

*Serikali; (i) kuharakisha utoaji dhamana isiyo ya fedha kwa mifuko ya pensheni (issuance of non cash bond) ili kuwezesha madeni yake kuingia katika kasma ya Deni la Taifa, (ii) kuweka utaratibu madhubuti wa kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa waliokiuka masharti ya dhamana na kuweka masharti magumu ya utaratibu wa utoaji dhamana hapo mbeleni;*

[1] ukuwaji unachangiwa na vitu vikuu vine – nakisi kubwa kwenye Bajeti ya Serikali, kuendelea kulipa deni la ndani kwa kukopa (rollover of liquidity papers), mikopo mipya, na kuporomoka kwa shilingi.

*(iii) ihakikishe kuwa taratibu zote za kukopa zinapitiwa na vyombo vyote muhimu ikiwa ni pamoja na "Technical Debt Manamegent Committe (TDMC)" na "National Debt Management Committee (NDMC)" kabla ya kusaini mikataba ya mikopo (iv) Waziri wa Fedha kupata ushauri/mapendekezo kutoka kwa Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Madeni(NDMC) kabla ya kusaini mikataba yoyote ya mkopo ili kuhakikisha mikopo imefata taratibu , sheria na masharti ni mazuri;(v) Kuzingatia mpango wa utoaji wa hati fungani katika kuingia mikopo ya ndani na nje (vi) Kuhakikisha bajeti ya Serikali ina uhalisia kuliko ilivyo sasa ili kupunguza nakisi ya bajeti na madeni (vii) kupitia na kurekebisha muundo wa Usimamizi wa Deni la Taifa uliopo hivi sasa (set up a unified debt management office).*

## 3.2 Ucheleweshwaji Michango ya Kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii-shilingi bilioni 284

Uhakiki wangu umebaini kuwa, makato ya kisheria ya jumla ya shilingi bilioni 284 yanayolipwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yalicheleweshwa kwa kipindi kati ya siku 30 mpaka siku 90 baada ya malipo ya mishahara ya mwezi. Ucheleweshwaji huu ulihusisha madai ya Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) kwa Serikali ya michango ya kabla ya 1999 (pre – 1999 pension obligations) pamoja na madai ya miaka ya nyuma kwa mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii.

Matokeo yake, nimebaini ucheleweshwaji mkubwa wa ulipaji wa mafao kwa wastaafu waliokuwa wakichangia kwenye mfuko wa pensheni kwa watumishi wa umma mwaka huu. Tatizo hili kilikuwepo kwa mifuko mingine ya hifadhi ya jamii. Ugumu wa maisha kwa wastaafu (wanufaika) unaotokana na kucheleweshaji wa malipo ya mafao yao ungepungua kama Serikali ingelipa malimbikizo ya madeni na michango yake kwa wakati hasa kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma.

***Ninaishauri Serikali kulipa malimbikizo ya madeni na michango yake kwa wakati kwa mifuko ili kuiwezesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutimiza majukumu yake ipasavyo na wastaafu kupata stahili zao kwa wakati.***

# 4.0 USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

**Ndugu Wanahabari,**

Udhaifu katika usimamizi wa rasilimali watu umeendelea kujitokeza katika ukaguzi wangu wa mwaka 2015/16 kama ifuatavyo:

## 4.1 Malipo ya mishahara ya shilingi bilioni 7.3 na makato ya kisheria ya shilingi bilioni 2.5 yalifanyika kwa watumishi walioacha kazi au kufariki

Ukaguzi wangu umebaini kuwa mishahara ya watumishi walioacha kazi, waliofariki, au waliostaafu, wameendelea kulipwa mishahara kupitia akaunti zao. Vilevile, fedha za makato ya mishahara ya watumishi hao zimeendelea kupelekwa kwenye taasisi husika kama vile Bima ya Afya ya Taifa, Mamlaka ya Mapato, Mifuko ya Jamii, n.k. Hali hii imesababishwa na watumishi hawa kuchelewa kutolewa katika orodha ya mishahara ya watumishi.
Jumla ya shilingi bilioni 1.2 kililipwa kwa sampuli ya watumishi 260 katika taasisi 19 za Serikali Kuu na shilingi Bilioni 6.1 zililipwa kwa watumishi katika Halmashauri 108 zilizokaguliwa.

Pia Makato ya mishahara hiyo ya jumla ya shilingi bilioni 2.2 ilikatwa kwa watumishi wasiokuwepo kazini kwa upande za Serikali za Mitaa na shilingi milioni 50.5 kwa upande wa Serikali Kuu. Hali hii bado inaendelea licha ya kuwa Serikali imewekeza kwenye mfumo wa LAWSON kama njia mojawapo ya kudhibiti udhaifu huo kujirudia.

Hata hivyo, kutokana na juhudi ambazo Serikali imezifanya katika kuhakiki orodha ya watumishi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16, hali hiyo inatarajiwa kupungua kwa mwaka ujao wa ukaguzi.

***Naishauri serikali iendelee kufanya ukaguzi endelevu wa rasilimali watu (manpower audit) mara kwa mara na kuhuisha orodha ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi wake.***

## 4.2 Kushindwa kujiridhisha kuhusu urejeshwaji wa Mishahara katika akaunti ya Hazina shilingi bilioni 4.33

Kutokana na Muongozo Na.03 uliotolewa na Hazina unaoamuru malipo ya mishahara kufanyika moja kwa moja katika akaunti za watumishi, ukaguzi wangu ulishindwa kujiridhisha kama kiasi kinachozuiliwa kufanya malipo kwa watumishi ambao hawako katika utumishi kinarejeshwa kunakostahili na benki husika. Katika sampuli ya Taasisi 8 za Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa 53, nilibaini jumla ya shilingi bilioni 4.33 hazikulipwa kwa wafanyakazi. Hata hivyo, sikuweza kuthibitisha kama kiasi hicho cha fedha kimerejeshwa Hazina na Benki husika.

***Serikali inashauriwa kuweka mfumo wa mrejesho, ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wote zitakuwa na uwezo wa kupata taarifa za zuio la malipo waliloweka kama limefika na kushughulikiwa na benki, ili kiasi kisicholipwa kiweze kurudishwa Hazina.***

### 4.3 Malimbikizo ya Madai ya Wafanyakazi kiasi cha Shilingi bilioni 14.4

Katika sampuli ya taasisi 7 za Serikali Kuu nilibaini malimbikizo ya madai ya wafanyakazi yanayofikia Shilingi bilioni 8.2 kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 10.

Vilevile, nilibaini malimbikizo yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni 6.2 kwa wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaofikia 5,225 katika sampuli ya halmashauri 13. Ucheleshwaji wa stahili za wafanyakazi unapunguza morali wa kazi.

***Ninaishauri Serikali kuhakikisha kuwa malimbikizo ya madai ya Watumishi yanawekwa kwenye bajeti na kulipwa ili kuinua ari ya watumishi kufanya kazi kwa bidii na ufanisi.***

### 4.4 Wakuu wa vitengo kukaimu nafasi zilizo wazi kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita

Ukaguzi wangu umebaini watumishi 49 katika Taasisi 14 za Serikali Kuu wakikaimu katika vyeo mbalimbali kwa zaidi ya kipindi cha miezi sita kinyume na Kanuni za kudumu za utumishi wa umma. Pia, hali hiyo ilijitokeza kwa watumishi 373 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 78.

***Ninaishauri Serikali kupunguza idadi ya maafisa wanaokaimu ama kwa kuwathibitisha wanaokaimu nafasi hizo endapo wana sifa stahiki au kufanya uteuzi wa maafisa wapya wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo.***

## 5.0 USIMAMIZI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA SERIKALI

**Ndugu Wanahabari,**

### 5.1 Matumizi yasiyokuwa na manufaa kwa Serikali Shilingi bilioni 2.02

Ukaguzi wangu umebaini matumizi yasiyokuwa na manufaa yenye jumla ya shilingi bilioni 1.46 kwa Serikali Kuu. Matumizi hayo yangeweza kuepukwa endapo Taasisi husika zingekuwa makini.

Kwa upande wa Serikali za mitaa, Halmashauri 14 zililipa jumla ya shilingi milioni 564.94 kwa taasisi husika. Mfano wa malipo hayo ni tozo mbalimbali, riba na gharama za usumbufu zinazojitokeza kutokana na kesi au kutotimiza masharti ya mikataba. Sababu zingine ni malipo yanayolipwa mara mbili.

***Naishauri Serikali kutekeleza majukumu yake ya mikataba ili kuepuka kufanya malipo yasiyokuwa na manufaa yoyote kwa Serikali. Pia,***

***kuimarisha udhibiti wa ndani katika kutekeleza majukumu yake ili kuondokana na migogoro mbalimbali isiyo na tija.***

**5.2 Kukosekana kwa nyaraka zinazothibitisha matumizi ya hamisho la fedha la shilingi bilioni 6.57**

Taasisi 4 za serikali kuu zilifanya malipo ya shilingi bilioni 6.57 ambazo hazikuthibitishwa kupitia ukaguzi wangu kwa sababu zilikosa nyaraka muhimu za malipo. Hivyo sikuweza kuthibitisha kama fedha hizo zilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

**5.3 Mapungufu katika nyaraka za malipo ya shilingi bilioni 22.7**

Ukaguzi umebaini mapungufu katika utunzaji wa nyaraka muhimu ikiwemo nyaraka za malipo. Wakati wa ukaguzi, Taasisi 29 za Serikali Kuu zilifanya malipo ya jumla ya shilingi bilioni 12.5. Hata hivyo, malipo hayo yalikosa nyaraka zinazothibitisha uhalali wa matumizi yaliyofanywa. Mapungufu katika nyaraka yanaathiri mawanda ya ukaguzi hivyo kuweza kusababisha kutolewa hati zisizoridhisha katika hesabu.

Kwa upande wa Serikali za Mitaa, Ukaguzi umebaini mapungufu katika utunzaji wa nyaraka muhimu ikiwemo nyaraka za malipo yenye jumla ya shilingi bilion 9.8. Hivyo, sikuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi yaliyofanywa na Halmashauri 109 kutokana na ufinyu wa mawanda ya ukaguzi.

***Ninaishauri Serikali kuimarisha udhibiti wa malipo ikiwa ni pamoja na kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa awali ili viweze kupitia kwa kina malipo yote kabla hayajafanyika. Pia, kuwe na utaratibu mzuri wa kutunza nyaraka za malipo na viambatanisho ili kusaidia kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.***

## 6.0 USIMAMIZI WA MALI NA MADENI YA SERIKALI

**Ndugu Wanahabari,**

**6.1 Uwepo wa Mali za kudumu zilizotelekezwa**

Ukaguzi wangu umebaini ongezeko la idadi ya magari yaliyotelekezwa katika taasisi mbalimbali za Serikali Kuu kutoka magari 675 mwaka 2014/15 hadi kufikia magari 1,272 mwaka 2015/16 (sawa na ongezeko la asilimia 88).

Kwa upande wa Serikali za Mitaa, jumla ya magari, pikipiki na mitambo inayofikia 652 yalitelekezwa pasipo hatua zozote kuchukuliwa na menejimenti. Aidha, kwa upande wa Idara na Wakala wa Serikali, jumla ya

magari 92 yalitelekezwa. Hata hivyo, menejimenti ya Taasisi husika haikuchukua hatua yoyote. Uwepo wa mali hizi kwa muda mrefu pasipo kuuzwa, unaweza kusababisha hasara itokanayo na wizi wa vifaa na uchakavu.

***Naishauri Serikali kuimarisha usimamizi wa mali za kudumu ili kuepusha uharibifu utokanao na kutelekezwa kwa mali hizo kwa muda mrefu.***

## 6.2 Dawa zilizokwisha muda wa matumizi ambazo hazijaharibiwa Shilingi bilioni 10.19

Kwa kwa upande wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Uhakiki wa dawa zilizonunuliwa kupitia fedha za Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, Ukimwi, na Kifua Kikuu uliofanyika kwenye ghala la Bohari Kuu ya Dawa umegundua uwepo wa dawa zilizokwisha muda wake zenye thamani ya Sh.10,187,671,563 ambazo ni mkusanyiko wa dawa hizo kwa miaka 12. Utunzaji wa dawa zilizokwisha muda wake kwa muda mrefu yanaongeza gharama za utunzaji.

***Ninaishauri Serikali iharakishe uteketezwaji wa dawa zilizokwisha muda wake kuondolewa kwa wakati kuepusha gharama za utunzaji na athari zinazoweza kujitokeza.***

**Ndugu Wanahabari,**

## 6.3 Ukarabati wa Majengo ya Serikali na uendelezwaji wa viwanja vya Serikali katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi

Kama nilivyobaini katika ukaguzi wangu uliopita, Serikali haijachukua hatua zozote kufanya ukarabati kwa baadhi ya nyumba katika Balozi za Tanzania nje ya nchi zilizo katika hali mbaya na hazifai kwa matumizi. Kati ya Balozi 34, balozi 12 zinamiliki nyumba 37 zilizo katika hali mbaya na zinahitaji marekebisho. Wakati huohuo, Serikali inamiliki viwanja 10 katika balozi mbalimbali ambavyo havijaendelezwa hivyo viko katika hatari ya kunyang'anywa.

***Ninaishauri Serikali itoe jukumu kwa taasisi moja itakayohusika na uendelezwaji wa viwanja na ukarabati wa majengo chakavu yaliyopo kwenye Balozi zetu.***

## 6.4 Miradi ya maendeleo iliyokamilika yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.2 ambayo haitumiki

Uhakiki wa matumizi ya miradi ya maendeleo iliyokamilika kwa baadhi ya Halmashuri ulibaini miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 4.2 ambayo haijaanza kutumika kutoa huduma kama ilivyokusudiwa. Walengwa

waliokusudiwa hawakupata faida iliyotarajiwa. Mfano wa miradi hiyo ni miradi ya maji ya visima na maji bomba, ambayo ilikamilika tangu mwaka 2013/14 katika Wilaya ya Simanjiro inayofikia thamani ya Shilingi milioni 985.21 na miradi ya maji iliyokamilika tangu mwaka 2014/15 katika Wilaya ya Nachingwea inayofikia thamani ya Shilingi Bilioni 1.66 ilikamilika lakini haikuwa inatumika.

***Ninaishauri Serikali kuhakikisha miradi iliyokamilika inaanza kutumika kama ilivyokusudiwa kwa faida ya wananchi.***

## 7.0 USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

**Ndugu Wanahabari,**

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2015/16 nimebaini mambo yafuatayo kuhusiana na usimamizi wa manunuzi:

**Jedwali Na. 4: Mapungufu katika manunuzi na mikataba**

| Mapungufu Husika | Idadi ya Taasisi | Kiasi cha fedha |
|---|---|---|
| Manunuzi yaliyofanyika bila ushindani kwa Serikali kuu | | shilingi bilioni 24.2 |
| Manunuzi yaliyofanyika bila Mikataba kwa serikali kuu | 10 | shilingi bilioni 11.2 na USD milioni 29.6 |
| Manunuzi kufanyika kwa wazabuni wasioidhinishwa na Mamlaka husika kwa serikali kuu | 14 | shilingi bilioni 7.3 |
| Manunuzi yaliyofanyika bila ushindani kwa serikali za mitaa | | shilingi bilioni 2.1 |
| Manunuzi kufanyika kwa wazabuni wasioidhinishwa na Mamlaka husika kwa serikali za mitaa | halmashauri 28 | shilingi bilioni 1.2 |
| Manunuzi yasiyoidhinishwa ya vifaa vya matibabu bila uthibitisho wa MSD kutokuwa na vifaa hivyo kwa serikali za mitaa | halmashauri 6 | milioni 72.78 |

***Ninaishauri Serikali kuzingatia matakwa ya Sheria za manunuzi ili kuepuka mapungufu yanayojitokeza.***

## 8.0 UKAGUZI WA VYAMA VYA SIASA

Ukaguzi wa vyama vya siasa ulibaini yafuatayo: (a) kukosekana kwa mchanganuo wa taarifa za fedha hivyo kunifanya nishindwe kujiridhisha kuhusu usahihi wa taarifa hizo; (b) vyama vya siasa vinne havikuandaa

taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi kama Kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa; (c) wafanyakazi wa vyama vya siasa hawakuwa na mikataba; na (d) vyama vya siasa vitatu havikuwa na akaunti za benki.

***Ninaishauri Serikali kupitia Msajili wa vyama vya siasa ahakikishe vyama vyote vilivyosajiliwa vina mfumo na rasilimali watu unaowezesha uandaaji wa hesabu zinazokidhi matakwa ya miongozo ya uhasibu.***

## 9.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA

### 9.1 Benki ya Wanawake Tanzania.

Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ilitoa Mikopo yenye jumla ya Shilingi milioni 655 bila kufata taratibu za utoaji wa mikopo kwa mfano kuthibitisha uwepo wa makampuni yaliyokopeshwa.

Aidha, nimebaini kwamba mtaji wa benki umepungua kulinganisha na kiwango kinachotakiwa kama Kanuni namba 5 ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Utoshelevu wa Mtaji – Capital Adequacy) ambayo inaitaka benki au taasisi ya fedha zenye ukomo wa maeneo ya kutoa huduma (with limited scope of services) kuanza kutoa huduma na kuhakikisha wakati wote zina kiasi cha chini cha mtaji kisichopungua shilingi bilioni 5.

***Benki ya wanawake Tanzania inashauriwa kuhakikisha inafuata matakwa ya kiwango cha chini cha mtaji kwa kufuatilia mwenendo wa mtaji kila siku na kuchukua hatua thabiti kudumisha kiwango cha chini cha mtaji.***

***Pia Benki Kuu ya Tanzania ifuatilie utendaji wa benki hii ili kuhakikisha kuwa haifilisiki.***

### 9.2 Benki ya Twiga

Katika kupitia uendelevu na uendeshaji wa benki ya Twiga nilibaini kwamba mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, benki ya Twiga katika mwaka unaoishia 31 Desemba 2015, ilikuwa na upungufu wa mtaji kwa wana hisa(negative equity) wenye thamani ya Shilingi bilioni 18.7. Hali hii inaleta mashaka juu ya uwezo wa benki hii kuendelea kujiendesha bila mashaka. Aidha, mtaji wa msingi wa benki katika miaka miwili ni chini ya kiwango cha chini kinachohitajika cha thamani ya shilingi bilioni 5 kinyume na matakwa Kanuni namba 5 ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha.

***Ninaishauri Serikali kufanya uchunguzi na kuainisha sababu zilizopelekea benki kufanya vibaya na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kubuni mikakati itakayosaidia utendaji wa benki kuimarika.***

## 9.3 Shirika la Usambazaji wa Umeme Tanzania (TANESCO)

(i) TANESCO ina malimbikizo makubwa ya madeni katika manunuzi ya umeme kutoka kwa watengenezaji huru wa nishati (IPPs) na Watengenezaji wa dharura wa nishati (EPPs).

Hii imesababishwa na TANESCO kununua umeme kwa bei ya wastani wa Shilingi 544.65 kutoka kwa IPPs/EPPs na kuuza kwa wastani wa Shilingi 279.35 kwa kila uniti hivyo kusababisha hasara ya wastani wa Shilingi 265.30 kwa kila uniti.

Jitihada zaidi zinahitajika kuliokoa Shirika katika hali liliyopo kwa kutafuta vyanzo mbadala vya umeme vyenye bei nafuu kama matumizi ya umeme unaozalishwa kwa maji na nishati ya gesi na kuachana na wazalishaji binafsi wanaotumia mafuta.

**(ii) Kuchelewa kutekeleza ujenzi wa mradi wa maji wa kuzalishia umeme katika korongo la Stiegler**

Mradi wa korongo la Stiegler ulikuwa katika mpango mkakati wa maendeleo ya sekta ya umeme wa mwaka 2012. Gharama kamili ya kujenga mradi huu ni Dola za Marekani bilioni 2.4.

Mapitio ya taarifa mbalimbali yanaonyesha kuwa mradi huu ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,100. Mpango mkakati wa sekta ya umeme wa mwaka 2012 unaonyesha kuwa mradi unatakiwa kujengwa kwa awamu tatu: Stiegler 1 megawati 300 - kukamilika 2024; Stiegler II megawati 600 - kukamilika 2026; na Stiegler III Megawati 300 - kukamilika 2028.

Hata hivyo nimebaini kuwa RUBADA inakabiliwa na changamoto ya kifedha kuweza kuuendeleza mradi.

***Ninashauri Serikali itafute fedha na kuwekeza kwenye mradi unaotegemewa kuwa wa bei nafuu zaidi ukilinganishwa na umeme unaotumiwa toka kwa makampuni binafsi ya uzalishaji umeme***.

## 9.4 Mifuko ya Pensheni

Nilibaini hali ya kushuka kwa mapato ya uwekezaji kwa kiasi kikubwa inayoikabili mifuko ya pensheni ya NSSF, PPF, PSPF na LAPF inatokana na kutokuwepo kwa ufanisi wa menejimeti katika kusimamia mikopo iliyotolewa kwa vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa, Usimamizi hafifu wa kuratibu shughuli za uwekezaji pamoja na kushindwa kukusanya madeni ya muda mrefu hii ikiwa ni pamoja na yale yanayodaiwa toka Serikalini yanayofikia Shilingi trilioni 1.6. Mapungufu haya yameanishwa kwa kina katika ripoti husika.

***Ninaishauri Serikali kusimamia mifuko ili iweze kufuata kanuni na mahitaji ya Sera zinazoongoza mifuko ya Hifadhi ya jamii ili kuongeza ufanisi. Serikali pia inashauriwa iongeze juhudi za kulipa madeni yake kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuipunguzia matatizo ya kifedha yanayoikabili.***

## 9.5 Mamlaka ya Bandari Tanzania

Ukaguzi Maalumu Kuhusu Malipo ya Ushuru wa bandari (wharfage) kwenye Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ulilenga kubaini waliohusika katika ukwepaji wa ushuru wa bandari na kubaini kiwango cha hasara iliyotokana na ukwepaji wa ushuru huo. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, ushuru wa Shilingi bilioni 15.02 haukukusanywa na Mamlaka ya Bandari kutokana na ubadhirifu wa makampuni ya kutoa mizigo bandarini, wafanyakazi wa Mamlaka ya bandari na watumishi wa mabenki.

***Ninaishauri Mamlaka ya Bandari kuhakikisha kwamba mapato yanayotokana na ushuru wa bandari yanakusanywa.***

## 9.6 Ukaguzi wa Sekta ya Madini

i. Ukaguzi wangu kwenye shughuli za mgodi wa Buckreef Gold Mine kupitia Mkataba wa ubia kati ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Kampuni ya TANZAM 2000 nilibaini kuwa mwaka 2011 TANZAM (2000) ililipa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 3 kwa STAMICO kama gharama za kununua asilimia 55 bila ya kuwa na vigezo vinavyotambulika kama uthaminishaji wa mali za mgodi kabla ya ubia. Zaidi ya hayo, tangu mwaka 2011 hadi wakati wa Ukaguzi huu, Machi, 2017 mgodi haujaanza kufanya kazi.

ii. **Kutoza Kodi kwa Kiwango cha Sifuri katika Kusafirisha Bidhaa za Madini Nje ya Nchi**

Mapitio ya malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka kwenye migodi mikubwa minne (4) ya dhahabu na mmoja wa Almasi kwa kipindi cha kati ya Mwaka 2012 mpaka 2016 yalibaini kuwa kulikuwa na marejesho makubwa ya kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,144.

Marejesho hayo makubwa yametokana na mianya inayotolewa na kifungu 55(1) cha sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya mwaka 2014, sawia na sheria za zamani, ambazo, zote kwa pamoja ziliruhusu na bado zinaruhusu tozo ya kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwa bidhaa zinazosafirishwa kuuzwa nje ya nchi.

Lengo la Serikali kutoza kodi ya ongezekeo la thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye bidhaa zote zinazosafirishwa kuuzwa nje ya nchi ilikuwa ni kukuza viwanda vya ndani, mapungufu yaliyojitokeza ni kuwa Sheria hiyo haikuweka makundi kuonyesha ni bidhaa zipi zinazostahili motisha hiyo. Hivyo basi madini ambayo kwa namna yoyote lazima yauzwe nje ya nchi nayo pia yananufaika na motisha hiyo kama vile ambavyo bidhaa za kilimo na viwandani zinavyonufaika.

***Serikali, kupitia STAMICO, inashauriwa kuhakikisha kuwa bei ya ununuzi ya migodi ya madini inayokubaliwa kwenye mikataba ya ushirikiano wa kibiashara sharti itokane na upembuzi wa kina, uthaminishaji wa mali au makadirio ya madini yaliyopo ardhini.***

***Serikali inashauriwa kupitia upya sheria ya kodi ya ongezeko la thamani ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho ili kuondoa tozo ya kiwango cha sifuri kwenye mauzo ya madini na vito nje ya nchi. Pia, kujadiliana na makampuni ya uchimbaji madini kuhusu matokeo ya mabadiliko hayo kwenye Mikataba yao (MDAs).***

### 9.7 Makampuni ya Madini Kutengeneza Hasara kwa Muda Mrefu

Mapitio ya taarifa za fedha na taarifa za malipo ya kodi za migodi ya dhahabu ya makampuni ya madini kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2012 mpaka 2016 yameonesha kuwa migodi imekuwa ikipata hasara mfululizo. Hasara hiyo, kwa kiasi kikubwa, imesababishwa na kuruhusiwa kupunguza kiasi chote cha gharama zitokanazo na manunuzi ya bidhaa za mtaji (capital expenditure) kutoka kwenye mapato ya uzalishaji kwa mwaka husika.

Mikataba mingi ya madini inaruhusu kupunguza gharama za manunuzi ya bidhaa za mtaji (capital expenditure allowances) kwa asilimia 80 hadi 100 katika mwaka ambao bidhaa imenunuliwa kuanzia hatua za utafiti mpaka uzalishaji. Hatua hii hupelekea kupata hasara mfululizo. Jedwali la hapa chini linaonesha baadhi ya makampuni makubwa ya madini yanavyopata hasara mfululizo kwa kipindi cha kati ya mwaka 2011 mpaka 2015.

**Jedwali Na. 5: Mchangauo wa jinsi makampuni makubwa ya uchimbaji madini Tanzania yanavyopata Hasara**

| Mwaka wa Fedha | Geita Gold Mine 'Shilingi bilioni | Bulyanhulu Gold Mines Ltd 'Shilingi bilioni | Pangea Minerals Ltd 'Shilingi bilioni | North Mara Gold Mine 'Shilingi bilioni | Williamson Diamond Ltd 'Shilingi bilioni |
|---|---|---|---|---|---|
| 2015 | 107.02 | (2,362.36) | (959.03) | (101.35) | (135.54) |
| 2014 | 77.75 | (2,047.71) | (727.47) | (234.35) | (106.56) |
| 2013 | 33.77 | (1,349.19) | (785.83) | (317.25) | (188.34) |
| 2012 | 219.17 | (182.95) | (8.21) | 75.91 | (107.51) |
| 2011 | 41.62 | (579.32) | (196.47) | 29.35 | - |
| | **479.34** | **(6,521.53)** | **(2,677.02)** | **(547.69)** | **(537.95)** |

*Chanzo: TRA*

***Serikali inashauriwa (a) kujadiliana na makampuni ya madini yanayopata hasara mfululizo ili Serikali iweze kutoza kodi kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mapato ghafi kulingana na aya ya 3(3) ya Jedwali la kwanza la sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 (toleo la 2015); (b) kuhakiki gharama za uwekezaji na marejesho ya kodi ili kuzuia matumizi mabaya ya misamaha ya kodi inayotolewa.***

## 9.8 Kuendelea Kutoza Kodi kwa Kiwango cha Chini Ikilinganishwa na Viwango Vinavyotozwa Sasa

Mikataba ya uchimbaji madini kati ya Serikali na makampuni ya uchimbaji katika migodi mingi ya dhahabu ilisainiwa kabla Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 haijatungwa. Viwango vya tozo za kodi katika mikataba hiyo vilitokana na sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1973 na havijabadilishwa kuendana na sheria mpya ya mwaka 2004 kutokana na kuwapo kwa kwa kifungu kinachozuia mabadiliko ya viwango vya tozo za kodi kwenye mikataba hiyo. Kwa mfano, mikataba hiyo inaainisha viwango vya zuio la kodi katika ada ya usimamizi pamoja na huduma za kiufundi kati ya asilimia 3 mpaka 5. Hii ni tofauti na asilimia 15 kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

***Serikali inashauriwa kujadiliana na makampuni ya uchimbaji madini kupitia kifungu kinachoruhusu kurejewa kwa mkataba kinachopatikana kwenye mikataba takribani yote ili kurekebisha viwango vya tozo za kodi kwa kuzingatia vigezo vya kiuchumi vinavyobadilika kufatana na muda tangu kusainiwa kwa mikataba hiyo.***

## 9.9 Ubia kati ya STAMICO na TML

Kampuni ya Sky Associates ilinunua hisa za umiliki wa kampuni ya TML inayoendesha mgodi wa Tanzanite toka kwa kampuni ya Richland Resources tarehe 30 Januari 2015.

Ukaguzi umebaini kampuni ya TML imekuwa ikiiuzia madini ya Tanzanite kampuni Tanzu ya Sky Associates bila kumshirikisha mbia mwenzake ambaye ni STAMICO.
Pia, nimebaini kuwa TML inatafuta masoko na kuuza Tanzanite bila kupata ukubali wa mshirika wake STAMICO ambayo ni kinyume na kifungu cha 15.1(b-d) cha makubaliano ya ubia kati ya STAMICO na TML.

***Ninaishauri Wizara ya Nishati na Madini, kupitia STAMICO, ihakikishe mauzo ya Tanzanite yanafanyika kwa uwazi mkubwa kupitia minada ya hadhara ili kuondoa nafasi zozote za kuuzwa kwa bei isiyo ya ushindani kati ya kampuni ndugu***

## 9.10 Tathmini ya Uendeshaji Mgodi wa STAMIGOLD - Biharamulo

Serikali, kupitia STAMICO, ilichukua mgodi wa dhahabu wa Tulawaka kutoka kwa kampuni ya Pangea Minerals Ltd. Mkataba wa kuhamisha umiliki ulifikiwa tarehe 15 Novemba, 2013. Ili kuendesha mgodi, STAMICO iliunda kampuni mpya kwa jina la STAMIGOLD. Tathmini yangu ya ufanisi wa mgodi chini ya usimamizi wa kampuni ya STAMIGOLD umeonyesha kuwa Wizara ya Nishati na Madini imecheleweshа kibali cha maandishi kabla umilikishwaji wa leseni kubwa ya kuchimba madini haijahamishwa kutoka kampuni moja kwenda nyingine kinyume na Kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Madini ya 2010.

***Ninaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kuharakisha mchakato wa kuipatia STAMIGOLD kibali cha kutumia mkataba wa kuchimba madini aliokuwa anautumia Pangea Minerals Ltd.***

## 9.11 Ukaguzi wa Mafuta na Gesi;

i. Ukaguzi ulibaini kuwa, matumizi ya bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ni ya kiwango cha chini cha ujazo kwa asilimia 94 huku TANESCO akiwa ndiye mteja pekee akitumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 ambayo ni sawa na asilimia 6 tu ya ujazo wa bomba husika licha ya kuwepo makubaliano kati ya TPDC na TANESCO ya kusambaza futi za ujazo milioni 138.8 katika vituo 6 vya kuzalisha umeme vya TANESCO.

ii. Pia nilibaini kuwa, Mkataba wa Ubia wa Uzalishaji wa Gesi (PSA) baina ya TPDC na Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited (PAET) umetengenezwa kwa namna ambayo gawio la Serikali kutoka kwenye mauzo ya gesi asilia litakuwa linapungua kadri uzalishaji unavyoongezeka kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:

**Jedwali Na. 6: Mchanganuo wa gawio la serikali linavyopungua kadri uzalishaji unavyoongezeka**

| **Wastani wa Mauzo kwa siku** | | **Ongezeko la mauzo kwa Gesi iliyoongezwa** | **Gawio la Faida ya mauzo ya gesi lililokubaliwa (%)** | |
|---|---|---|---|---|
| **Mita za ujazo Millioni kwa siku (mmcfd)** | | **Mita za Ujazo Billion (BCF)** | **TPDC** | **PAET** |
| 0 hadi 20 | | 0 to 125 | 75 | 25 |
| Zaidi ya 20 ila pungufu kuliko au sawa na 30 | **OR** | Zaidi ya 125 ila pungufu kuliko au sawa na 250 | 70 | 30 |
| Zaidi ya 30 ila pungufu kuliko au sawa na 40 | | Zaidi ya 250 ila pungufu kuliko au sawa na 375 | 65 | 35 |
| Zaidi ya 40 ila pungufu kuliko au sawa na 50 | | Zaidi ya 375 ila pungufu kuliko au sawa na 500 | 60 | 40 |
| Zaidi ya 50 | | Zaidi ya 500 | 45 | 55 |

Mkataba huu hauitaki Pan African Energy Tanzania Limited kulipa mrahaba kwa serikali badala yake TPDC ndiyo hulipa mrahaba huo. PAET pia inakata kodi zote kutoka katika mapato yake kama gharama za uendeshaji na uwekezaji na hivyo kuifanya PAET kutolipa kodi yoyote kwa serikali katika kipindi chote cha mkataba.

***Napendekeza kufanyika upya kwa makubaliano ya mgawanyo wa uzalishaji (PSA) ili kuiwezesha Serikali kunufaika zaidi pindi uzalishaji unapoongezeka. Pia ninaishauri Serikali kupitia Wizara ya Madini, TPDC na TANESCO kujadiliana namna nzuri ya kukamilisha mitambo ya uzalishaji wa umeme ili bomba la gesi litumike kwa ufanisi.***

**(iii) Kukosekana kwa Kifungu cha Kutozwa Kodi ya Ziada Katika Sheria ya Kodi 2004.**

Ukaguzi ulibaini kuwa kifungu cha 13.1(a) cha Ibara ya XIII ya mkataba wa ushirikiano wa uchimbaji gesi ya eneo la Songosongo kinaitaka PAET kulipa kodi ya ziada ya faida (Additional Profit Tax) ambayo inatakiwa kulipwa kulingana na mkataba kila mwaka na itategemea faida halisi inayopatikana kutokana na mzunguko wa fedha kwenye mkataba husika.

Sambamba na hayo, nilibaini PAET haijawahi kuwasilisha ripoti ya kodi ya ziada ya faida (statements of additional profit tax).

Hata hivyo, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 haikuwa na kipengele cha kodi la Ongezeko la Faida, Mawasiliano na uongozi wa TRA yameonyesha kuwa sheria hii bado inaandaliwa.

Ni maoni yangu kwamba, kukosekana kwa kifungu cha kutozwa kodi ya ziada kunasababisha Serikali kukosa kodi kutoka kwenye chanzo hiki cha mapato.

***Napendekeza Serikali kupitia upya makubaliano ya mikataba na kufanya marekebisho ili iweke vifungu vinavyohusika na kutozwa kwa kodi ya ziada. Pia, Sheria ya Kodi ya Mapato inatakiwa ibadilishwe ili ijumuishe tozo la kodi ya ziada.***

## 10.0 MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU

**Ndugu Wanahabari,**

### 10.1 Ukaguzi maalumu wa Mamlaka ya Vitabulisho vya Taifa

Ukaguzi umejiridhisha kwamba uongozi wafanyakazi na watoa huduma na wazabuni wameshiriki kwa namna moja au nyingine katika ubadhirifu na udanganyifu kwenye matumizi ya fedha katika mradi wa kuboredha Vitambulisho vya Taifa. Mradi huu unajumuisha mikataba ya manunuzi ya vifaa vya kuboresha Vitambulisho vya taifa, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kama vile ipad, programu na Vifaa vya kompyuta, upatikanaji wa vibarua, bima za magari na gharama za kusafirisha na kufunga vifaa vya kusajili raia ambapo, shilingi bilioni 4.5 zilikuwa na udanganyifu.

Zaidi ya hayo, kutokana na hali ya usajili na kutoa vitambulisho vya taifa kuwa mpya, hali hiyo ilisababishwa na maandalizi hafifu kwa uongozi wa Mamlaka juu ya kuamua jinsi mfumo ambao ungeweza kutumika vizuri kulingana na uwezo wa Mamlaka.

Hali hiyo ilisababisha mabadiliko ya maelekezo yaliyoigharimu Serikali kupitia manunuzi yasiyo na tija na wakati huo huo wadanganyifu kutumia mianya iliyopo kujinufaisha wenyewe kinyume na taratibu.

### 10.2 Ukaguzi Maalum wa Fedha za Gavi Alliance Kwa Ajili ya Chanjo ya Surua Rubella

Kutokana na ukaguzi maalum, udhaifu mkubwa ulionekana katika mfumo wa udhibiti wa ndani. Udanganyifu na viashiria vya rushwa katika maeneo ya manunuzi, masurufu, matumizi ya fedha na uendeshaji wa ruzuku kwa ujumla.
Ilibainika wakati wa ukaguzi maalum kwamba memoranda ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na GAVI Alliance ilikiukwa kwa sababu msaada huo kwa ajili ya chanjo haukuwekwa kwenye Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF).

Pia, haukufuata taratibu za Serikali za kuhamisha fedha kupitia hazina ndogo na baadaye kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA).

Mapungufu mengine ni pamoja na: (a) fedha ambazo hatukuweza kufahamu matumizi yake shilingi 2,153,289,221; (b) Shilingi 1,077,167,188 zilizotumwa Serikali za Mitaa hazikuthibitishwa kupokelewa; (c) ununuzi wa mafuta kwa ulaghai shilingi 248,034,893; (d) malipo ya shilingi 1,192,493,345 yaliyofanywa kwa halmashauri 54 na hospitali za mikoa 11 kwa ajili ya shughuli mbalimbali hayakuwa na nyaraka za kuthibisha uhalali wake; (e) Shilingi 497,182,500 kilitumika kwa ajili ya mafunzo ya Surua Rubella bila kuwa na nyaraka za kuthibitisha hilo; (f) matumizi ya shilingi 316,292,995 kwa ajili ya chakula yalikuwa na nyaraka za kughushi; (g) timu ya ukaguzi haikuweza kuthibitisha ukarabati na matengenezo ya magari kiasi cha shilingi 137,743,754; na (h) Mafuta ambayo hayakuthibitika matumizi yake katika leja ya stoo shilingi 372,398,769.

Maelezo zaidi kuhusu kaguzi hizi yanapatikana katika sura ya kumi na mbili ya Serikali Kuu.

## 11.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA UFANISI

### 11.1 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi

**Ndugu Wanahabari,**

Ripoti hii ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo 107 yaliyotolewa katika Ripoti Tano za Ukaguzi wa Ufanisi zilizowasilishwa Bungeni katika kipindi cha mwaka 2012 na 2013. Ufuatiliaji wa mara kwa mara wa utekelezaji wa mapendekezo unasaidia kuhakikisha kuwa mapendekezo yaliyotolewa yanatekelezwa kiufasaha na kwa wakati ili kuleta tija zaidi katika utendaji wa serikali. Ilibainika kuwa kati ya mapendekezo 107 yalitolewa, mapendekezo 40 yalitekelezwa kikamilifu; mapendekezo 37 yalitekelezwa kwa kiasi; na mapendekezo 30 hayakutekelezwa kabisa (**Jedwali 1**).

**Jedwali 1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi**

| Ripoti ya Ukaguzi | Jumla ya mapendekezo yaliyotolewa | Idadi ya Mapendekezo yaliyotekelewa Kikamilifu | Idadi ya Mapendekezo yaliyo tekelezwa Kiasi | Idadi ya Mapendekezo yasiyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|
| Usimamizi wa ukaguzi unaofanywa na Askari wa usalama barabarani pamoja na Udhibiti wa mwendo kasi nchini (2012) | 25 | 11 | 4 | 10 |
| Usimamizi wa Mikataba ya Miradi ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa (2013) | 11 | 0 | 2 | 9 |
| Usimamizi wa Ununuzi wa vifaa vya Teknohama katika Sekta ya Umma (2013) | 20 | 6 | 5 | 9 |
| Usimamizi wa Afya na Usalama mahali pa kazi (2013) | 27 | 20 | 6 | 1 |
| Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria (2013) | 24 | 3 | 20 | 1 |
| **Jumla** | 107 (100%) | 40 (37%) | 37 (35%) | 30 (28%) |

Kwa ujumla utekelezaji wa mapendekezo niliyotoa hauridhishi hususani ikizingatiwa kuwa ni asilimia 37 tu ya mapendekezo hayo yametekelezwa kikamilifu. Sehemu iliyobaki ya mapendekezo hayo ama hayajatekelezwa kabisa au utekelezaji wake bado unaendelea ingawa hadi sasa ni wastani wa miaka 4 hadi 5 tangu mapendekezo hayo yatolewe. Ilibainika kuwa utekelezaji umekuwa si wa kuridhisha kutokana na taasisi za umma

kutokuwa na mfumo madhubuti wa kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi.

## 11.2 UKAGUZI WA UFANISI – MAFUTA NA GESI ASILIA

**Ndugu Wanahabari**

- ***Asilimia 9 tu ya pesa iliyotumiwa katika manunuzi ya sekta ya mafuta na gesi ilikwenda kwa makampuni ya Kitanzania***

Imebainika kuwepo kwa mfumo dhaifu wa kusimamia utekelezaji wa kanuni za kuwashirikisha wazawa katika sekta ya mafuta na gesi. Hakuna sera, kanuni au taratibu zinazosimamia utekelezaji wa vifungu vinavyotaka ushirikishaji wazawa kutoka katika mikataba ya kugawana mapato (PSA's). Katika kipindi cha kati ya mwaka 2011 hadi 2014, makampuni ya kitanzania yalipata mikataba yenye thamani ya asilimia 9 kati ya jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 2 zilizotumiwa na makampuni ya kimataifa ya mafuta katika manunuzi mbalimbali.

- ***Hakuna udhibiti wa mchakato wa ugawaji leseni za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi***

Sheria na kanuni zilizopo hazijaweka taratibu sahihi za ugawaji wa leseni na mikataba ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa makampuni ya kimataifa ya mafuta na gesi. Aidha, hakuna udhibiti unaohakikisha kwamba mchakato wa ugawaji leseni unaendana na sheria za manunuzi zilizopo.

- ***Asilimia 6 pekee ya idadi ya wataalamu katika sekta ya mafuta na gesi wamepewa mafunzo yaliyokusudiwa***

Imebainika uzalishaji wa wataalamu haukidhi mahitaji ya sasa ya wataalamu wa kada mbalimbali katika sekta ya mafuta na gesi. Kwa ujumla serikali imeweza kutekeleza asilimia 20 ya malengo yake katika utekelezaji wa mipango ya programu za mafunzo ya muda mrefu. Aidha, katika kipindi cha miaka 4 (2012-2016) serikali ilitoa mafunzo kwa asilimia 6 tu kati ya idadi iliyopangwa kwa ngazi ya wataalamu na mafundi watenda kazi. Kuna upungufu wa asilimia 48 ya watoaji mafunzo kama ilivyojionesha kutoka katika taasisi kuu 6 za mafunzo zilizoteuliwa kuongoza utoaji wa elimu na ujuzi katika sekta ya mafuta na gesi.

- ***Ukusanyaji wa mapato ya kodi chini ya wastani katika sekta ya mafuta na gesi***

Hakuna ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanyo na shughuli za uchimbajii wa mafuta na gesi. Kwa hivi sasa kiasi cha mapato yanayokusanywa kutoka katika sekta ya mafuta na gesi ni chini ya wastani na serikali bado haijafanikiwa kufikia uwezo wake wa juu katika ukusanyaji

wa mapato yatokanayo na kodi katika sekta ya mafuta na gesi. Kwa miaka 4 kati ya 5 iliyopita Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya chini ya wastani wake wa shilingi za Kitanzania Bilioni 208.

- ***Hatari ya kuharibu ubora, usahihi na kiwango cha taarifa za kijiolojia na kijiofizikia***

Shirika la Maendeleo ya Petroli halina udhibiti kamili wa ubora, usahihi na kiwango cha taarifa za kijiofizikia na kijiolojia wanazosimamia. Kuna hatari ya kuharibu ubora, usahihi na kiwango cha taarifa kwa sababu ya kukosekana kwa mfumo madhubuti wa usimamizi wa taarifa za kijiolojia na kijiofizikia. Aidha kuna hatari ya kutoa tafsiri isiyo sahihi na matokeo yanayopotosha kutokana na kutokuwa na utaalamu madhubuit wa kuchakata na kuchambua taarifa za kijiolojia na kijiofizikia.

- ***Asilimia 4 pekee ya miradi ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi imekaguliwa kukidhi kanuni za uhifadhi wa mazingira***

Ripoti zimeonesha kwamba hakuna ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya mafuta na gesi kuangalia iwapo inakidhi kanuni za uhifadhi wa mazingira zilizowekwa wakati wa utoaji wa ithibati za tathmini za madhara kwa mazingira. Katika kipindi cha miaka 5 kati ya 2010-2015 kulikuwa na jumla ya miradi 71 iliyosajiliwa katika utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi ambapo kati ya hiyo ni asilimia 4 pekee ndiyo iliweza kukaguliwa iwapo inakidhi masharti ya utunzaji wa mazingira.

**Mapendekezo**

- ***Wizara ya Nishati na Madini** Kufanya upembuzi wa kina kwa kushirikiana na wadau muhimu ili kubainisha mapungufu ya ujuzi/utaalamu pamoja na fursa za ajira kwa Watanzania kwenye sekta ya mafuta na gesi ambapo mahitaji halisi yatabainishwa;*

    - *Pia, Kuandaa mpango mahususi na wa kina wa uandaji wa mipango na mikakati ya uendelezaji wa rasilimali watu ambao utatatua mahitaji ya utaalamu na ujuzi unahitajika katika kila hatua ya mnyororo wa thamani kwenye sekta ya mafuta na gesi na kuhakikisha kuwa inatekelezwa na matokeo yake kupimwa na kuwasilishwa kwa wadau muhimu kwenye sekta ya umma na binafsi;*

    - *Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini iweke mkakati wa kupima ongezeko kwa pato la Shirika la Maendeleo ya Petroli ili kushiriki kwenye biashara na shughuli za utafutaji, uendelezaji, na uzalishaji wa mafuta na gesi nchini;*

- ***Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania k**uandaa mfumo wa usimamizi wa sera ambao utatumika kutoa mwelekeo wa usimamizi wenye ufanisi wa taarifa za kijiofizikia na kijiolojia;*

- ***Ofisi ya Makamu wa Rais - Kurugenzi ya Mazingira kuhakikisha** Shughuli za udhibiti na usimamizi wa mazingira zinazofanywa na Baraza*

*la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, wizara za kisekta na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinaratibiwa, zinaoanishwa, na kwamba mfumo wa utoaji wa taarifa unaimarishwa baina ya wadau wote wa sekta ya mafuta na gesi kwenye upande wa mazingira;*

- ***Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira linatakiwa*** *Kuweka viwango na vigezo vya utendaji katika shughuli za usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya vihatarishi, miongozo ya udhibiti na usimamizi, na muda utakaotumika katika kila shughuli ya udhibiti na usimamizi kwenye sekta ya mafuta na gesi;*
- ***Mamlaka ya Mapato Tanzania k****uandaa mfumo wa kuweka malengo ya ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye sekta ya mafuta na gesi ili kupima kwa usahihi utendaji na matokeo ya shughuli za ukusanyaji wa mapato.*
- ***Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi k****uandaa mpango wa kina wa shughuli zinazohusu ukuzaji wa ujuzi. Mpango huo unatakiwa kushirikisha na kueleweka na wadau kama vile taasisi za elimu, mamlaka za udhibiti na wizara za kisekta ambazo zina jukumu katika ukuzaji wa ujuzi kwenye sekta ya mafuta na gesi.*

## 11.3 RIPOTI UKAGUZI WA UFANISI KATIKA UZALISHAJI WA WAHITIMU KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**Ndugu Wanahabari,**

- ***UDHAIFU WA MIPANGO NA MIKAKATI KWA AJILI YA KUZALISHA UJUZI KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA***

Wizara ya Elimu haikuwa na mipango na mikakati thabiti kwa kwa ajili ya kuzalisha ujuzi katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Hii ni kwa sababu Wizara ya Elimu haikufanya uchambuzi wa kina kutambua mahitaji ya ujuzi unaotakiwa katika mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi asilia. Pia, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Vyuo Vikuu na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi hawajafanya ufuatiliaji na tathmini ya kutosha ya shughuli za kutoa ujuzi katika sekta ya mafuta na gesi asilia kwa kipindi cha miaka mitatu toka mwaka 2012/13 - 2015/16.

- ***UWEZO MDOGO WA TAASISI ZOTE SITA ZINAZOTOA ELIMU NA MAFUNZO KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI NCHINI***

Taasisi sita za elimu na mafunzo nchini hazina uwezo wa kutosha wa kuzalisha wahitimu wenye ujuzi unaohitajika katika sekta ya mafuta na gesi asilia kutokana na mapungufu yafuatayo:

**Asilimia 45 ya ujuzi za kitaalamu zinazohitajika zinakosekana kwenye mitaala ya vyuo vikuu vinavyotoa elimu katika sekta ya mafuta na gesi**

**asilia**: Mitaala inayotumika katika vyuo vikuu inakosa takribani ujuzi 10 za kitaalamu sawa na asilimia 45 ya ujuzi zinazotakiwa katika ngazi ya vyuo vikuu.

**Asilimia 69 ya ujuzi wa kitaalamu zinakosekana kwenye mitaala ya vyuo vya ufundi vinavyotoa elimu katika sekta ya mafuta na gesi asilia**: Kati ya ujuzi 16 unaohitajika katika ngazi ya vyuo vya ufundi stadi na ufundi, takribani ujuzi 11 sawa na asilimia 69 unakosekana kwenye mitaala hiyo;

**Asilimia 33 tu ya vyuo zinatoa kozi ya afya, usalama mahali pa kazi na mazingira:** Kati ya taasisi sita zinazotoa mafunzo na elimu kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia, ni taasis 2 (33%) zinatoa kozi ya afya, usalama mahala pa kazi na mazingira. Japokuwa kozi hii ni muhimu kumwezesha mhitimu kuweza kuajiriwa katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

- ***UKOSEFU WA MIUNDOMBINU NA VIFAA KWA AJILI YA KUTOA MAFUNZO YA VITENDO***

Vyuo vyote sita vilivyokaguliwa vinakabiliwa na upungufu wa vifaa na miundombinu kwa ajili ya kutoa mafunzo kama vile maabara, vifaa na zana kwa ajili ya kufanya mafunzo ya vitendo. Kati ya vyuo hivyo sita, vyuo 2 (33%) havikuwa na maabara kwa ajili ya kutoa mafunzo ya vitendo. Pia vyuo vitatu (50%) vinakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya maabara. Kadhalika, vyuo vyote sita vinakabiliwa na upungufu wa vitabu na vifaa vya kisayansi kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

- ***UPUNGUFU WA WAKUFUNZI***

Katika vyuo sita vinavyotoa elimu ya mafuta na gesi asilia nchini, vinaupungufu wa wakufunzi kati ya asilimia 8 hadi asilimia 56, kama ilivyo kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali: Asilimia inayoonyesha upungufu wa Wakufunzi kwenye vyuo Sita vinavyotoa elimu ya mafuta na gesi asilia**

| Jina la Chuo | Idadi ya Wakufunzi Wanaohitajika | Idadi ya Wakufunzi waliopo | Kiasi cha upungufu wa Wakufunzi (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (CONAS,CoET na UDBS) | 19 | 8 | 56 |
| Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) | 16 | 7 | 56 |
| Chuo Cha Madini Dodoma (MRI) | 18 | 16 | 11 |
| Chuo Cha Madini Shinyanga (ESIS) | 6 | 3 | 50 |
| Chuo cha Ufundi Stadi VETA- Lindi | 12 | 7 | 42 |
| Chuo cha Ufundi Stadi VETA-Mtwara | 12 | 11 | 8 |

**Mapendekezo:**

- ***Ninapendekeza kwamba Wizaya ya Elimu iangalie upya mfumo mzima wa kusimamia shughuli za uzalishaji wa ujuzi unaohitajika katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Hii ni pamoja na kuandaa mipango kwa ajili ya kusimamia shughuli zinazohusu kukuza ujuzi, kuandaa mfumo sahihi wa ufuatiliaji, uratibu na mawasiliano na pia kuhakikisha kuna upatikanaji endelevu wa fedha za kutekeleza shughuli hizo.***

- ***Pia ninapendekeza Wizara ya Elimu ihakikishe kuwa Tume ya Vyuo Vikuu na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi waandae utaratibu wa kufuatilia na kuhakikisha mitaala ya Taasisi za Elimu na mafunzo inaandaliwa kwa ufanisi, taasisi za mafunzo zina vifaa vya mafunzo na zinaweza kutoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi.***

## 11.4 RIPOTI YA UKAGUZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MSINGI

**Ndugu Wanahabari,**

- ***KUTOKUFUATWA TARATIBU ZA USAJILI WA SHULE KUMECHANGIA UPUNGUFU WA MIUNDOMBINU***

Asilimia 94 ya shule zilizoanzishwa nchini zinatoa huduma bila ya kusajiliwa na Wizara ya Elimu. Shule hizo zimekuwa zikitoa huduma licha ya kuwa na upungufu mkubwa wa miundombinu. Ukaguzi umebaini wanafunzi wapatao milioni 3.7 sawa na asilimia 48 ya wanafunzi wote nchini hawana madarasa ya kusomea na wanafunzi milioni 5.2 hawana vyoo. Ukosefu wa vyumba vya madarasa umesababisha madawati yapatayo 243,000 kuhifadhiwa nje huku yakiharibiwa na mvua, jua au yamekuwa yanarundikwa kwenye chumba kimoja cha darasa.

- ***UKAGUZI WA SHULE ZA MSINGI HAUKAGUI MIUNDOMBINU KWA KINA***

Ukaguzi wa shule umekuwa ukifanyika kinyume na mipango iliyowekwa. Aidha, hata kaguzi chache ambazo zilizofanyika hazikuweza kuzingatia na kujumuisha mambo ya miundombinu. Kutokana na hali hiyo, shule zote ambazo hazikukaguliwa zimeendelea kutoa haduma licha ya kukosa miundombinu inayohitajika pasipo kupewa adhabu ya aina yoyote na Wizara ya Elimu.

- ***BAJETI HAFIFU YA UJENZI NA UKUKARABATI WA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MSINGI***

Serikali iliweka mikakati ya kutenga wastani wa asilimia 22 ya bajeti kwa kila mwaka kwa ajili ya matumizi ya sekta ya elimu. Lakini bajeti hii imepunguwa kutoka asilimia 19 kwa mwaka 2012/13 hadi asilimia 17 katika mwaka wa fedha wa 2013/14, 2014/15 na 2015/16. Hii imesababisha uwepo

wa majengo chakavu katika shule za msingi na kushindwa kujenga miundombinu mipya ili kuenda sambamba na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na shule za msingi.

**Mapendekezo**

- ***Ninashauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuweka mfumo utakao hakikisha shule zote za msingi nchini zinasajiliwa kulingana na taratibu zilizowekwa; ianzishe utaratibu wa kukagua miundombinu ya shule za msingi na kwa wakati. Pia, ifuatilie mara kwa mara utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa.***

- ***Ofisi ya Rais - TAMISEMI kutenga rasilimali fedha na kuweka mfumo wa kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinatumika ipasavyo katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi; Pia iweke mfumo yakinifu wa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na wadhibiti ubora wa shule za msingi hasa yale yanayohusiana na uwepo na ukarabati wa miundombinu.***

## 11.5 RIPOTI YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU UDHIBITI WA UENDELEZAJI WA MAENEO YA WAZI YAALIYOAINISHWA NCHINI

**Ndugu Wanahabari,**

- ***ASILIMIA 86 YA MIPANGO MIJI ILIYOTEMBELEWA HAIJAANZA MCHAKATO WA USAJILI WA MAENEO YA WAZI***

Imebainika Mipango Miji sita (6) kati ya saba (7) iliyotembelewa haijaanza utaratibu wa kusajili maeneo ya wazi ya umma ili kutambuliwa umiliki licha ya kukumbushwa na TAMISEMI kupitia barua ya kumbukumbu CAB.39 / 156/01/13 ya tarehe 23 Oktoba 2014 na CAB.39 / 156/01/27 ya Januari 20, 2015 iliyowataka Mamlaka ya Mipango Miji kuhakikisha wana hati ya kumiliki ardhi kwa ardhi yote ya umma chini ya usimamizi wao ifikapo tarehe 30 Januari 2015.

- ***MAENEO YA WAZI 573 HAYAJASAJILIWA***

Ukaguzi ulibaini kuwa jumla ya maeneo ya wazi 573 katika Mamlaka ya Mipango Miji saba iliyotembelewa hayajasajiliwa. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo: Halmashauri ya Jiji la Arusha (50); CDA (33); Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni (157); Halmashauri ya Jiji la Mbeya (122); Halmashauri ya Manispaa ya Moshi (86); Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara (58); na Halmashauri ya Jiji la Mwanza (67). Pia maeneo hayo ya wazi hayakuwa na hati miliki na hivyo kuweza kusababisha Halmashauri kushindwa kuthibitisha umiliki, uvamizi wa maeneo hayo na pia kukatisha tamaa wenye nia ya kuendeleza (potential developers).

- *MAENEO YA WAZI 302 YAMEVAMIWA*

Ilibainika jumla ya maeneo ya wazi 302 kati ya 573 ya Mipango Miji iliyotembelewa yamevamiwa na wananchi. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo: Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni (157); Halmashauri ya Jiji la Mbeya (122); Halmashauri ya Manispaa ya Moshi (86); na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara (58).

Pia ilibainika kuwa maeneo ya wazi 55 (Halmashauri ya Jiji la Mbeya - 20; Halmashauri ya Manispaa ya Moshi - 2; na CDA - 33) yamebadilishiwa matumizi na hivyo kuendelezwa kinyume na mpango wa awali. Kwa mfano maeneo ya umma ya wazi 17 (52%) chini ya CDA yaliidhinishwa na kubadilishiwa matumizi na kuwa baa yenye majengo ya kudumu; maeneo ya umma ya wazi 10 (30%) yamewekwa minara ya simu na maeneo ya umma ya wazi 6 (18%) yameidhinishiwa matumizi mengine.

**Mapendekezo**

- ***Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhakikisha kuwa inandaa mipango madhubuti ili maeneo ya wazi yote yawe na hati miliki;***
- ***kuhakikisha kuwa mamlaka za upangaji zinakuwa na utaratibu mzuri wa kukagua maeneo ya wazi yaliotengwa;***
- ***inafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa kwa wavamizi wa maeneo ya wazi;***
- ***na kuhakikisha jamii inaeleweshwa umuhimu na matumizi ya maeneo ya wazi kijamii, kiuchumi na kimazingira ili waweze kuyaheshimu, kuyatunza na kuyalinda.***

## 11.6 UKAGUZI WA UFANISI KATIKA USIMAMIZI WA USALAMA DHIDI YA MOTO KATIKA MAJENGO YA UMMA

**Ndugu Wanahabari,**

- *MAJENGO YA UMMA HAYAKUKAGULIWA KWA ZAIDI YA MWAKA*

Ukaguzi ulibaini kwamba kati ya majengo 20 yaliyotembelewa, 3 (asilimia 15) hayakukaguliwa kwa zaidi ya mwaka na matokeo yake Jeshi halikuweza kutambua kuzingatiwa kwa matakwa ya usalama dhidi ya moto kwa wamiliki wa majengo hayo. Pia jengo 1 lilipewa cheti cha usalama dhidi ya moto pasipo kuwa yamezingatia usalama dhidi ya moto kinyume na matakwa ya sheria.

- ***JESHI HALIKUBAINISHA KIKAMILIFU MAPUNGUFU YALIYOONEKANA WAKATI WA UKAGUZI.***

Ukaguzi ulibainisha kwamba, kati ya majengo 20 yaliyokaguliwa, majengo 11(asilimia 55) yalibainika kuwa na vifaa vya kuzimia moto vilivyoisha muda wa kutumika na kukosa vifaa vya kung'amua (kutambua) uwepo wa moshi. Pia, kati ya majengo 14 yaliyokaguliwa, jengo 1 (asilimia 7) njia ya dharula ya kutokea wakati wa moto ilikuwa imefungwa na majengo 7 Kati ya 11 (asilimia 64) hayakuwa na mabomba ya mipira kwa ajili ya kuzimia moto. Hivyo, wamiliki wa majengo kushindwa kuboresha hali ya kuzingatia usalama dhidi ya moto kwani mapungufu hayakubainishwa wakati wa ukaguzi. Hali hii ilisababisha hatari kubwa ya kupoteza mali na maisha pindi moto unapotokea kwani kwa mikoa iliyotembelewa, athari kubwa ilikuwa kwa mkoa wa Dar es Salaam ambapo watu 40 walifariki na 38 walijeruhiwa. Hali hii ilitokana na mkoa wa Dar es Salaam kuwa na matukio mengi ya moto kuliko mikoa mingine.

- ***KUFANYIKA KWA UKAGUZI USIO NA UBORA NA PASIPO KUBAINISHA MASUALA YA MSINGI***

Masuala makuu yanayotakiwa kuzingatiwa kwa ukaguzi bora ni; ukaguzi unatakiwa kuangalia eneo husika lote, kubaini mapungufu yote yaliyopo na kutoa mapendekezo kadri ya ukaguzi ulivyofanyika. Ukaguzi ulibaini kwamba, kati ya majengo 21 yaliyotembelewa, 8 (asilimia 38) yalikuwa na mapungufu ambayo hayakubainishwa katika taarifa ya ukaguzi. Baadhi ya mapungufu hayo ni; vifaa vya kuzimia moto visivyofanyiwa matengenezo baada ya kuisha muda wa kutumika; uwekaji usio kamilika wa mabomba ya maji kwa ajili ya kuzimia moto; kutokuwekwa kwa vifaa vya kung'amua (kutambua) moshi; na kuzibwa kwa njia za dharula za kutokea wakati wa moto. Matokeo yake masuala ya msingi ambayo huongeza mazingira magumu ya kwa usalama dhidi ya moto hayakubainishwa.

- ***UWASILISHAJI DUNI WA MATOKEO YA UKAGUZI KWA WAMILIKI WA MAJENGO***

Ukaguzi ulibaini kwamba, Jeshi la Zima Moto na Uokoaji haliwasilishi ipasavyo matokeo ya ukaguzi kwani taarifa hazioneshi mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi na mapendekezo yaliyotolewa hayaoneshi viwango vya ubora wa vifaa vinavyotakiwa kuwekwa yaani maelezo ya kina ya kifaa, ukubwa na asili ya kifaa kinachotakiwa kuwekwa ambapo kati ya mikoa minne ya Jeshi iliyotembelewa, mikoa miwili ilionesha mapungufu ya vifaa. Hii inamaanisha kwamba, hata kama ukaguzi unafanyika na mapendekezo hutolewa bado wamiliki wa majengo hawatawezi kuweka vifaa sahihi kwa ajili ya kujikinga dhidi ya moto.

- ***JESHI LA ZIMA MOTO NA UOKOAJI KUTOPITIA NA KUIDHINISHA MICHORO YA MAJENGO***

Ilibainika kuwa Jeshi halipitii michoro ya ujenzi na kutoa idhini wakati wa mchakato wa uidhinishaji wa michoro ya ujenzi unaofanywa na halmashauri za serikali za mitaa. Pia Jeshi halichukui hatua za kuwakataza wananchi kujenga majengo pasipo idhini ya Jeshi na kusababishwa majengo kujengwa pasipo kuzingatia matakwa ya usalama dhidi ya moto na kuwa na majengo yasiyo na usalama dhidi ya moto.

- ***JESHI LA ZIMA MOTO NA UOKOAJI HALIFUATILII KIKAMILIFU UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KITAALAMU***

Ukaguzi ulibaini kuwa, Kati ya majengo 15 yaliyotembelewa, ufuatiliaji ulifanyika kwa jengo 1 ( asilimia 7) tu na ufuatiliaji ulifanyika miezi miwili baada ya kupita kwa muda uliooneshwa kwenye taarifa kwamba Jeshi litaenda kufanya ufuatiliaji. Ilibainika pia hakukuwa na ufuatiliaji wa utekelezaji wa ushauri wa utaalamu kwa majengo yaliyokaguliwa hadi kipindi ukaguzi huu ulipofanyika. Hali hii husababisha wamiliki kusuasua kufanyia kazi mapendekezo waliyopewa kwa kukosa msukumo wa Jeshi.

**Mapendekezo**

- ***Ninashauri Jeshi la Zima Moto lifanye ukaguzi kikamilifu ili kuweza kubainisha mapungufu yaliyopo na kutoa ushauri uliokamilifu, hii ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa ushauri wa kitaalamu unafanyika na kutoa adhabu stahiki kwa wakiukaji wa matakwa ya usalama dhidi ya moto.***

- ***Jeshi la Zimamoto lishirikiane na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuunda mfumo utakao hakikisha kwamba michoro yote ya ujenzi inapitiwa na Jeshi kabla ya kuidhinishwa; Pia Jeshi la Zimamoto liimarishe ukaguzi wa majengo ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa ushauri wa kitaalamu.***

## 11.7 USIMAMIZI WA MIKATABA ILIYOINGIWA KATI YA SERIKALI NA HOSPITALI ZA BINAFSI NCHINI

**Ndugu Wanahabari,**

- ***MAHITAJI KUTOCHAMBULIWA KABLA YA KUINGIA MIKATABA***

Ilibainika Serikali haikuweka mipango stahiki kabla ya kuingia mikataba na hospitali za binafsi, ikiwemo kufanya uchambuzi wa mahitaji pamoja na kutathmini uwezo wa hospitali zilizokusudiwa, ili kuzifanya ziweze kutoa huduma kama hospitali teule za kanda na wilaya. Hii ilisababisha uwepo wa hospitali mbili katika halmashauri moja zinazotambuliwa na halmashauri husika kuwa ni za wilaya.

- ***M**IKATABA KUTOTATHMINIWA TANGU ISAINIWE*

Ilibainika uwepo wa mikataba baina ya Serikali na Hospitali teule iliokaa muda mrefu bila ya mapitio kuona kama bado inalinda maslahi ya umma licha ya uwepo wa mabadiliko kupitia Mwongozo wa ushirikiano wa Taasis za Umma na Binafsi katika Sera ya Afya 2013. Mwongozo wa 2013 unataja vigezo vya kuzingatia kuwepo katika mkataba ambavyo ni kipindi cha makubaliano (lifespan of the agreement), wigo wa huduma, mapitio (review), kuvunjwa mkataba au hatua za kuchukua kutokana na kuvunja makubaliano.Baadhi ya mikataba imetekelezwa kwa zaidi ya miaka 20 tangu iliposainiwa.

| **Hospitali** | **Taasis ya Serikali iliyoingia mkataba** | **Miaka toka mkataba kusainiwa** |
|---|---|---|
| Bugando | Wizara ya Afya | 31 |
| KCMC | Wizara ya Afya | 25 |
| Sumve | Halmashauri ya Kwimba | 25 |
| Machame | Halmashauri ya Hai | 5 |
| Nyangao | Halmashauri ya Lindi | 3 |
| CCBRT | Wizara ya Afya | 3 |
| Kolandoto | Manispaa ya Shinyanga | 3 |
| Kibosho | Halmashauri ya Moshi | 2 |

- ***B**EI ELEKEZI ZA HUDUMA ZA AFYA ZIMEPITWA NA WAKATI NA HIVYO KUTOFUATWA*

Serikali ilitoa mwongozo wa uchangiaji gharama mwaka 1997 ulioambatana na bei elekezi za huduma za afya. Hospitali zote zilipaswa kufuata bei hizi. Hata hivyo, bei hizi hazijawahi kufanyiwa mapitio kwa miaka 20.

Matokeo yake, hospitali zimekuwa zikiweka bei za huduma kama zilivyoona inafaa. Kwa mfano, katika hospitali za kanda, bei za sasa ni kati ya mara 28 na 720 ya bei elekezi. Katika hospitali teule za wilaya, bei za sasa nia katika ya mara 5 na 44 ya bei elekezi.

**Mapendekezo**

***Ninashauri Wizara ya Afya iandae mwongozo wa uingiaji wa mikataba utakaotumika katika kuandaa mikataba. Pia isimamie ipasavyo Utekelezaji wa mikataba ikiwa ni pamoja na kuifanyia tathmini mara kwa mara.***

***Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe tathmini yakutosha inafanyika ili kubaini kama hospitali inayopendekezwa kutumika kama teule ya halmashauri inakidhi vigezo.***

## 11.8 UKAGUZI WA UFANISI KATIKA USIMAMIZI WA SAMANI ZA BARABARANI

**Ndugu Wanahabari,**

- ***ASILIMIA 50 YA BARABARA HAZIKUZINGATIA MAHITAJI YA KIUSALAMA KWA WATUMIAJI WA BARABARA***

Ukaguzi umebaini ya kwamba Wakala wa barabara hawakuhusisha ipasavyo wadau kama vile polisi wa usalama barabarani, maafisa wa mipango miji pamoja na jamii zinazoishi kandokando ya barabara wakati wa kuandaa mipango ya uwekaji wa samani barabarani. Hii imesababisha asilimia 50% za barabara zilizopitiwa na wakaguzi kubainika kuwa hazikufuata kanuni za usalama wa barabarani kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wakati wa uwekaji wa samani za barabarani. Hii imetokana na TANROADS kutofanya tathmini ya mahitaji ya watumiaji wa barabara husika.

- ***SHILINGI MILIONI 309.75 ZILIZOTENGWA KWA UNUNUZI WA SAMANI ZA BARABARANI KWA WALEMAVU HAZIKUTUMIKA KAMA ILIVYO PANGWA***

TANROADS ilitenga Shilingi milioni 309.746 kwa ajili ya ununuzi wa samani za watu wenye ulemavu katika mikoa nane iliyopitiwa wakati wa ukaguzi. Imebainika kuwa alama za walemavu hazikuwekwa kama ilivyotakiwa, ukiondoa mkoa wa Iringa ambao walitekeleza zoezi hili kwa asilimia 100, mikoa mingine saba iliyobaki (Dar es salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Dodoma, Mbeya na Mtwara) walikua chini ya asilimia 30 ya utekelezaji.

- ***ASILIMIA 92 YA KAGUZI ZA USALAMA BARABARANI HAZIKUFANYIKA KAMA INAVYOTAKIWA***

Kati ya kaguzi 66 za usalama barabarani zilizotakiwa kufanyika, wizara pamoja na TANROADS wamefanya kaguzi 5 (8%) tu zilifanyika kati ya mwaka 2012 mpaka 2016. Hata hivyo, zaidi ya asilimia 75 ya mapendekezo yaliyotolewa kwenye kaguzi tano zilizofanyika hayakutekelezwa, hivyo fedha iliyotumika kwa ajili ya shughuli hii haikutimiza malengo kusudiwa. Kutofanyika kwa kaguzi za usalama, kumeathiri uwezo wa TANROADS na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kushindwa kutambua kwa wakati mahitaji ya kiusalama barabarani ambazo zinahitajika.

- ***MIGOGORO KUHUSIANA NA USIMAMIZI WA HIFADHI ZA BARABARA NA UWEKAJI WA MABANGO YA BIASHARA KATIKA MAENEO YA MIJINI***

Ilibainika uwepo wa migogoro kati ya TANROADS na Halmashauri mbalimbali katika mikoa nane yote ya ukaguzi huu. Migogoro hii inahusiana na uwekaji

wa mabango ya biashara katika hifadhi ya barabara kuu hasa zinazopita mijini. Hii inatokana na halmashauri kuruhusu uwekaji wa mabango mjini kwa mujibu wa sheria ndogondogo zao, ilhali TANROADS wanasimamia Mwongozo wa Hifadhi za Barabara wa mwaka 2016 na sheria nyinginezo zinazohusu usimamizi wa Barabara.

- *VIPENGELE VYA USALAMA BARABARANI KUTOZINGATIWA WAKATI WA UWEKAJI WA SAMANI ZA BARABARANI*

Usimamizi dhaifu wa miradi ya barabara wakati wa uwekaji samani pamoja na ukaguzi dhaifu wakati wa makabidhiano ya barabara vimechangia barabara nyingi kukosa samani stahiki na zenye ubora unaotakiwa. Katika hili, ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa alama na michoro katika baadhi ya maeneo hatarishi ya barabara kama vile katika miteremko mikali na katika maeneo yenye mikunjo mikali. Alama za barabarani, michoro pamoja na kingo za usalama zilibainika chini ya kiwango. Mfano, vibao vingi vilibainika kuwa vimetengenezwa kwa kutumia zege badala ya chuma. Pia michoro imeonekana kuchorwa kwa rangi zisizo rasmi kwa michoro au mistari ya barabarani hivyo kupauka mapema au kufutika kabisa.

**Mapendekezo**

- ***Nashauri Wakala wa Barabara (TANROADS) kuhakikisha kwamba wadau muhimu wa usalama barabarani wanahusishwa katika mipango ya uwekaji na matengenezo ya samani za barabarani.***

- ***Wakala wa Barabara kuimarisha usimamizi wa miradi ya barabara katika kila hatua ya mradi wa barabara ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji ya watumiaji wa barabara kabla na baada ya miradi.***

- ***Wizara ya Ujenzi pamoja na Wakala wa Barabara kuweka mfumo wa ufuatiliaji utakaotoa mwongozo wa mtiririko wa taarifa kwa ufanisi baina ya taasisi zinazohusika na uwekaji na matengenezo ya samani za barabarani.***

## 11.9 USIMAMIZI WA UCHUKUAJI WA MAJI KUTOKA KATIKA VYANZO VYA MAJI

**Ndugu Wanahabari,**

- *KUTOKUWEPO KWA MPANGO JUMUIFU*

- Imebainika kutokuwepo kwa mpango jumuifu wa usimamizi wa rasilimali za maji *(Integrated Water Resource Management and Development Plan)*. Hii ilisababisha mipango ya mgawanyo wa maji

usiozingatia kiasi cha maji kilichopo *water balance)*. Kwa sabuabu hii hata vibali vilivyotolewa havikuzingatia kiasi cha maji kilichopo.

- *MATUMIZI YA MAJI KUTOKA KWENYE VYANZO BILA KIBALI*

Imebainika watumiaji walitoa maji kutoka katika vyanzo mbalimbali bila kuwa na vibali kutoka kwenye Bodi za Mabonde ya Maji husika kutokana na vyanzo ya maji kutokaguliwa ipasavyo. Kwa watumiaji wenye vibali, hakukuwa udhibiti wa kuthibitisha kuwa watumiaji walitumia maji bila kuzidisha viwango walivyoruhusiwa. Watumiaji wenye vibali walitumia maji mengi kuliko viwango vilivyoainishwa katika vibali. Kwa mfano, MWAUWASA ilizidisha maji kwa asilimia 70 (ilitumia mita za ujazo 90,000 badala ya 53,000). Bodi ya Bonde ilistahili kupata Shilingi milioni 40.5 kama malipo ya ziada lakini hazikulipwa.

Katika mapitio ya taarifa ya ukaguzi mdogo uliofanywa na Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu mwaka 2015, katika wilaya ya Ilala tu, ulibaini uwepo wa visima holela visivyosajiliwa 2626, na vilivyosajiliwa vilikuwa 262 pekee. Kutokuwepo kwa ukaguzi wa mara kwa mara umepelekea ongezeko la watumiamaji holela bila ya kuwa na vibali rasmi kutoka katika Bodi za Maji za mabonde husika. Kama visima hivyo holela 2626 vingechimbwa kwa kufuata utaratibu rasmi, bonde la Maji la Wami/Ruvu wangepata jumla ya shilingi za kitanzania zinazo kadiriwa kufikia shilling milioni 814.

Ukaguzi wa vyanzo vya maji haukufanyika ipasavyo kwani maeneo mengi matumizi ya maji yamefanyika bila kuwa na vibali kutoka kwenye mabonde ya maji husika. Aidha ukaguzi umebaini kuwa kutokana na ukaguzi mdogo wa vyanzo vya maji, hata wale wenye vibali vya utumiaji maji nao pia hutumia kiasi cha maji kikubwa zaidi tofauti na kiasi kilicho ainishwa kwenye vibali vyao.

- *UDHAIFU KATIKA UKUSANYAJI WA MADUHULI*

Kulikuwa na udhaifu katika ukusanyaji wa maduhuli ya matumizi ya maji, na kusababisha kuwepo madeni makubwa hasa kwenye taasisi za serikali na mamlaka za usambazaji maji za miji na vijiji. Mabonde manne yaliyofanyiwa ukaguzi yameweza kukusanya Shilingi bilioni 2.6 kati ya bilioni 5.1 (51%) walizokuwa wanadai katika kipindi cha 2011/2012 hadi 2015/2016. Kati ya fedha hizi, taasisi za serikali zinadaiwa Shilingi bilioni 1.2 Hii ilisababisha Bodi za Mabonde kukosa fedha za kutekeleza baadhi ya majukumu yao.

Aidha imebainika kuwa hatua zinazochukuliwa dhidi ya watumia maji wasiofuata sheria sio madhubuti na hii imesababisha watumia maji bila kufuata sheria kuongezeka, hivyo kuvihatarisha vyanzo vya maji.

- *UWEPO WA JUMUIYA CHACHE ZA WATUMIA MAJI*

Ukaguzi ulibaini uwepo wa jumuiya chache za watumia maji katika mabonde ya Maji yaliyo tembelewa. Hii imepelekea ugumu katika ukusanyaji wa maduhuli ya matumizi ya maji na pia ugumu katika utatuzi wa migogoro baina ya watumia maji wa eneo husika.

| Bonde | Idadi ya jumuiya za watumia maji zilizo kusudiwa kuanzisha | Idadi ya jumuiya za watumiamaji zilizoanzishwa |
|---|---|---|
| Bonde la kati | 18 | 3 |
| Bonde la ziwa Victoria | 29 | 7 |
| Bonde la Pangani | 30 | 13 |
| Bonde la Wami/Ruvu | 33 | 15 |

- ***UWEPO WA JUMLA YA VITUO VYA HALI YA HEWA VIBOVU 18 KATI YA 30 KATIKA MABONDE YA WAMI/RUVU NA ZIWA VICTORIA***

Ilibaini kuwa Wizara ya Maji haikuweza kutoa msaada wa kiufundi katika mabonde ya Wami/Ruvu na Ziwa Victoria hivyo kupelekea uwepo wa vituo vya hali ya hewa visivyofanya kazi 10 kati 12 vilivyopo tangu mwaka 2014 katika bonde la maji la Wami/Ruvu, na pia 8 kati ya 18 katika bonde la ziwa Victoria. Taarifa za ubovu wa vituo hivyo ziliwasilishwa wizarani japo wizara husika ilishindwa kutoa msaada unaohitajika. Hii imeathiri upatikanaji na uchakatuaji wa taarifa za awali ambazo ni muhimu katika kujua kiasi cha maji kinacho patikana eneo husika.

- ***MIPANGO YA MATUMIZI YA MAJI BILA KUZINGATIA SHERIA YA MAJI YA 2009***

Kwenye mabonde yote yaliyotembelewa hapakuwa na utekelezaji wa mipango ya utumiaji wa maji kama inavyoelekezwa na sheria namba 11 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya 2009, pamoja na Sera ya Maji ya mwaka 2002. Mipango iliyokuwepo ilitegemea uhitaji wa maji pekee, hivyo vipengele muhimu kama mizania ya maji na akiba ya maji kwa ajiri ya mazingira havikuzingatiwa, hii ilipelekea uwepo wa migogoro kati ya watumia maji wa juu na wa chini.

Aidha sheria inataka mipango ya matumizi ya maji iwe shirikishi kwa kuwahusisha wadau wote wa maji, lakini ukaguzi ulibaini kuwa kwa kipindi chote cha miaka mitano wadau hawakushirikishwa katika mipango ya utumiaji maji. Ingawa kumekuwa na mchakato wa kuandaa mpango wa pamoja wa matumizi ya rasilimali maji ambao ukikamilika utasaidia ushirikishwaji wa wadau wote. Japokuwa mpaka sasa haijajulikana kwa uhakika ni lini mpango huo utaanza kutumika katika mabonde yote.

### Mapendekezo

- ***Ninapendekeza kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ikamilishe mpango wa usimamizi jumuifu wa rasilimali maji na kuutekelza ipasavyo katika bodi zote za mabonde yote ya maji.***

- ***Bodi zote za Mabonde ya Maji zipewe wataalamu na vitendea kazi vya kutosha kwa ajiri ya shughuli za ukaguzi na usimamizi wa vyanzo vya maji.***

- ***Pia ninapendekeza kuwa, Bodi za Mabonde ya Maji ziimarishe mifumo ya ukusanyaji maduhuli ili kufanikisha shughuli za usimamizi wa vyanzo vya maji.***

## 11.10 USIMAMIZI WA KAGUZI ZA VYOMBO VYA MAJINI KWA AJILI YA KUPEWA VYETI VYA UBORA NA KUKIDHI VIWANGO VYA USALAMA WA USAFIRISHAJI

**Ndugu Wanahabari,**

- ***KUKOSEKANA KWA KANZIDATA YA KUSAJILI MELI NDOGO***

Imebainika SUMATRA kutokuwa na rejesta kwa ajili ya meli ndogo. Hii imesababisha kushindwa kuzitambua meli zote na pia namba moja ya usajili kutolewa kwa zaidi ya meli moja.

| Namba ya usajili | Jina la Meli | Tarehe ya usajili |
|---|---|---|
| TAN0001 | LADY DIANA 4 | 16.04.2012 |
| | LADY DIANA | 09.05.2013 |
| | MV.DELGADO | 27.10.2014 |
| TAN00013 | MV.KIJISEHEMU | 26.05.2015 |
| | FIBRE | 10.05.2012 |
| TAN008 | MV. PEPI | 08.05.2012 |
| | MV.ZABAR JADA | 02.03.2015 |
| TAN00015 | MV.MTELEZI | 26.05.2015 |
| | KAMCHEZO | 10.05.2012 |
| LND 001 | MV. MAPUJU | Haikuwepo |
| | MV. MTANENA | Haikuwepo |

- ***ZAIDI YA ASILIMIA 80 YA MELI NDOGO KUTOKUKAGULIWA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE.***

Ukaguzi ulibaini kuwa katika kipindi cha 2012/2013 – 2015/2016, zaidi ya asilimia 80 ya meli ndogo hazikukaguliwa kabisa kama inavyooneshwa kwenye jedwali

**Jedwali linaloonesha kiwango cha meli ndogo ambazo hazikukaguliwa katika kipindi cha 2012/13-2015/16**

| Mwaka | Sensa ya meli ndogo (2012) | Idadi ya meli ndogo zilizo kaguliwa | Asilimia ya meli ndogo zilizokaguliwa (%) | Asilimia ya meli ndogo ambazo hazikukaguliwa (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2011/12 | - | 4,825 | N/A | N/A |
| 2012/13 | 30,866 | 6,156 | 20 | 80 |
| 2013/14 | 30,866 | 4,634 | 15 | 85 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2014/15 | 30,866 | 4,502 | 15 | 85 |
| 2015/16 | 30,866 | 3,748 | 12 | 88 |

- ***MELI ZENYE MAPUNGUFU KUTOCHUKULIWA HATUA STAHIKI***

katika kipindi cha mwaka 2015/16 SUMATRA ilifanyanya kaguzi ya meli na kubaini meli 1,667 zikiwa na mapungufu. Hata hivyo ni meli 31 (2%) ndizo zilichukuliwa hatua wakati meli 1,636 hazikuthibitishwa hatua stahiki zilizochukuliwa. Wakati mwingine, meli zilizogunduliwa kuwa na mapungufu ziliruhusiwa kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji.

- ***UPOTEVU WA ZAIDI YA BILIONI 4.5 ZA KITANZANIA KAMA MAPATO KWA KUTOKUSANYA USHURU WA KUSAJILI UPYA MELI NDOGO.***

Ukaguzi ulibaini upotevu wa mapato ambayo yangekusanywa kama ushuru wa kusajili upya meli ndogo ambazo hazikukaguliwa na SUMATRA ungefanyika. Upotevu huo wa mapato, unakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi za kitanzania zaidi ya 4.5 bilioni kwa kipindi cha mwaka 2012/13 hadi 2015/16

**Mapendekezo**

- ***Ninapendekeza SUMATRA Ifanye tathmini ya utekelezaji wa mipango yake kuhusiana na ukaguzi wa vyombo vya majini kwa lengo la kufanya maboresho. Pia, iweke mfumo utakao hakikisha meli ndogo zinasajiliwa na kupewa leseni na kutunza taarifa hizo katika kanzidata.***

- ***Napendekeza Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuweka mfumo wa utoaji taarifa utakaohakikisha utoaji wa taarifa za SUMATRA kuhusu usalama wa usafirishaji majini ikiwa ni pamoja na kuweka kipaumbele katika ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa SUMATRA hususani katika ukaguzi wa vyombo vya majini.***